*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

# Uelekeo

| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00061 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Aprili 24 - 30, 2024 |




**Dk. Mwinyi: Serikali kuajiri walimu wapya, kuboresha maslahi yao**



Uk. 3

**Saratani ya mlango wa kizazi kinara kuwatesa Watanzania**



Uk. 8

**Jinsi chumvi inavyoathiri mwili na kusababisha magonjwa**



Uk. 18

# Nchimbi afunguka mazito uchaguzi

- Kila chama kipewe nafasi kwa uzoefu wake
- CCM ipewe heshima kuendelea kuongoza nchi
- Upinzani upewe heshima kuendelea kupinga



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Balozi wa Rwanda nchini Tanzania, Fatou Harerimana alipokwenda Ikulu Chamwimo mkoami Dodoma kuaga baada ya kumaliza muda wake wa kazi.nchini jana.

## TAKUKURU yafuatilia miradi ya bilioni 61/-

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kinondoni, Dar es Salaam, imefanikiwa kufuatilia utekelezaji miradi sita yenye thamani ya zaidi ya Sh. Bilioni 61 ikiwemo mradi wa ujenzi wa uwanja michezo Mwenge ambao umekamilika kwa asilimia 92. **Uk. 4**

## Samia avutia wazawa kuwekeza nchini



**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), limesema katika muda wa miaka mitatu ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan madarakani, kumekuwepo na ongezeko kubwa la wazawa kuwekeza nchini. **Uk. 4**

**ALI HASSAN MWINYI: Muungano kama ndoa, haikosi migongano** Uk. 11

# Watoto 60 wafanyiwa upasuaji moyo Kambi Maalum JKCI

**Na Mwandishi Maalum**

WATOTO 60 waliozaliwa na matatizo ya moyo ambayo ni matundu na mishipa ya damu kutokukaa katika mpangilio wake, watafanyiwa upasuaji wa moyo katika kambi maalum ya matibabu Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI).

Kambi hiyo ya upasuaji mkubwa na mdogo wa moyo ya siku nane, inafanyika chini ya wataalamu wa JKCI kwa kushirikiana na wenzao kutoka mradi wa Little Heart wa Shirika la Muntada Aid lenye makao yake makuu jijini London, Uingereza.

Mkuu wa Kitengo cha Magonjwa ya Moyo kwa Watoto wa JKCI, Dk. Sulende Kubhoja, alisema katika kambi hiyo, watoto wanafanyiwa uchunguzi na wanaokutwa na matatizo wanafanyiwa upasuaji mdogo wa moyo kwa njia ya tundu dogo kupitia mtambo wa Cathlab pamoja na upasuaji mkubwa wa moyo wa kufungua kifua.

"Tunawaomba wazazi wenye watoto wanaosumbuliwa na matatizo ya moyo yakiwemo matundu, mishipa ya damu na valvu za moyo (PDA, ASD, VSD for device closure na PS), wawalete JKCI kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi na kupata matibabu.

"Pia tunawaomba madaktari kutoka hospitali zote nchini, kuwapa rufaa watoto wenye matatizo hayo ili waje JKCI kwa ajili ya kupata huduma za matibabu," alisema Dk. Kubhoja ambaye pia ni Daktari Bingwa wa magonjwa ya moyo kwa watoto.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Idara ya Upasuaji, Dk. Angela Muhozya, Daktari Bingwa wa upasuaji wa moyo wa JKCI, Alex Joseph, alisema wanatarajia kufanya upasuaji mkubwa wa kufungua kifua kwa watoto 20.

> **Mgonjwa anayefanyiwa upasuaji mkubwa wa moyo, anahitaji damu nyingi, tunashukuru tuna damu ya kutosha kwa ajIli ya watoto wanaofanyiwa upasuaji, tunawaomba wananchi muendelee kuchangia damu kwa ajili ya watoto wetu wanaofanyiwa upasuaji wa moyo.**

"Mgonjwa anayefanyiwa upasuaji mkubwa wa moyo, anahitaji damu nyingi, tunashukuru tuna damu ya kutosha kwa ajlli ya watoto wanaofanyiwa upasuaji, tunawaomba wananchi muendelee kuchangia damu kwa ajili ya watoto wetu wanaofanyiwa upasuaji wa moyo," alisema Dk. Alex.

Kwa upande wake, Daktari Bingwa wa magonjwa ya moyo kwa watoto wa JKCI, Stella Mongela, alisema katika kambi hiyo, watoto 40 watafanyiwa upasuaji mdogo wa moyo kwa njia ya tundu dogo kupitia mtambo wa Cathlab.

"Katika upasuaji huu mdogo wa moyo, tunatumia mtambo wa Cathlab ambao ni maabara maalum inayotumia mionzi kwa ajili ya kufanya uchunguzi na matibabu ya moyo, matibabu tunayoyatoa ni ya kuziba matundu ya moyo pamoja na kuzibua mishipa ya damu ya moyo iliyoziba," alisema.

Naye Meneja wa Miradi wa Shirika la Muntada Aid, Kabir Miah, alisema shirika hilo lina miradi mingi ikiwemo ya afya, elimu na maji na linafanya kazi katika nchi mbalimbali duniani ambapo katika Bara la Afrika, linafanya kazi katika nchi 30 ikiwemo Tanzania.

"Hii ni mara ya tisa tunakuja Tanzania kuwasaidia watoto wenye matatizo ya moyo na tumeshafanya upasuaji kwa watoto 475, tunafurahi kuona tumeokoa maisha ya watoto ambao baada ya kupona, wanaendelea na maisha yao kama watoto wengine ambao hawakuzaliwa na matatizo ya moyo," alisema Kabir.

# Tanzania yaongoza Afrika idadi kubwa ya simba, nyati na chui





**Na Mwandishi Maalum**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki, amesema Tanzania inaongoza kwa kuwa na simba, nyati na chui wengi barani Afrika, huku ikishikilia nafasi ya tatu kwa kuwa na idadi kubwa ya tembo.

Akitangaza matokeo ya sensa ya wanyamapori juzi ambapo pia alizindua taarifa ya watalii wa kimataifa waliotembelea Tanzania mwaka 2023, Waziri Angellah alisema matokeo ya sensa hiyo yatasaidia kwenye usimamizi wa wanyamapori nchini na kupanga mipango ya kuboresha uhifadhi na kutangaza utalii duniani.

Sensa ya wanyamapori ilifanywa na Tawiri kwa kushirikiana na Tanapa, Tawa, NCAA, Idara ya Wanyamapori na Frankfurt Zoological Society katika mifumo ya ikolojia ya Nyerere-Selous-Mikumi, Saadani-Wamimbiki na Serengeti.

Matokeo hayo ya sensa yalitangazwa kwenye mkutano uliowahusisha wadau wa uhifadhi na utalii.

Alisema tayari serikali imetenga fedha kwa ajili ya kufanya sensa ya wanyamapori nchi nzima mapema hapo mwakani.

Aliitaka Tawiri kuandaa mpango kazi kwa ajili ya sensa ijayo huku pia akielekeza watendaji wa wizara yake kuchambua kwa kina matokeo ya sensa hii ili yaleta tija.

Akitoa taarifa ya sensa hiyo, alisema spishi zilizoonyesha idadi kubwa ni pamoja na nyati (59,878), tembo (20,006), nyumbu (19,060), kongoni (18,361), swalapala (14,031) na ngiri (13,806), ambapo spishi zilizoonyesha idadi ndogo ni pamoja na twiga (1,679), tandala mkubwa/ kudu (1,414) na puku/ sheshe (496).

Alisema kwa upande wa tembo, idadi imeongezeka kutoka 15,501 (2018) hadi 20,006 (2022) na viashiria vya ujangili wa tembo au vifo vya tembo vimepungua kwa kiasi kikubwa hadi asilimia 0.8 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 16 wakati wa sensa ya 2018.

Akizungumzia taarifa ya watalii wa kimataifa walioitembelea Tanzania mwaka jana alisema Sekta ya Utalii ni miongoni mwa sekta muhimu katika uchumi wa dunia na imeendelea kuimarika baada kuathiriwa na mlipuko wa janga la Uviko-19.

Alisema mwaka jana sekta ya utalii duniani iliimarika kwa kiwango cha asilimia 88 ikilinganishwa na kiwango cha juu kilichofikiwa mwaka 2019.

"Hali hii ilitokana na ukuaji endelevu wa maendeleo ya teknolojia na juhudi za kukuza na kuendeleza maeneo mengine ya utalii duniani. Takwimu zinaonyesha kuwa idadi ya watalii duniani iliongezeka kwa asilimia 34 hadi kufikia watalii bilioni 1.3 mwaka jana kutoka milioni 960 mwaka juzi," alisema.

Alisema kwa Tanzania, utalii wa kimataifa umeimarika kwa kiwango cha asilimia 118.4 mwaka jana ikilinganishwa na kiwango cha juu kabla ya janga la Uviko-19.

Aidha, alisema idadi ya watalii wa kimataifa iliongezeka kutoka watalii milioni 1.4 mwaka juzi hadi kufikia watalii milioni 1.8 mwaka jana sawa na ongezeko la asilimia 24.3.

"Hatuna budi kutambua kazi kubwa aliyoifanya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, aliyeitangaza Tanzania kupitia filamu ya Tanzania The Royal Tour," alisema.

# Dk. Mwinyi: Serikali kuajiri walimu wapya, kuboresha maslahi yao

**Na Mwandishi Wetu, Zanzibar**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi, amesema serikali itaajiri walimu wapya wa masomo ya sayansi na itaendelea kuboresha maslahi yao.

Rais Dk.Mwinyi alisema hayo alipofungua Skuli ya ghorofa ya Sekondari Hassan Khamis Hafidh iliyopo Monduli Wilaya ya Magharibi A Mkoa wa Mjini Magharibi juzi ikiwa ni maadhimisho ya miaka ya 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Aidha, aliiapongeza Wizara ya Elimu kwa kazi nzuri ya kuvuka malengo ya Ilani ya Utekelezaji ya Uchaguzi ya CCM 2020-2025.

Kadhalika, Rais Dk. Mwinyi alifafanua kuwa ujenzi wa miundombinu ya skuli ina lengo la kuboresha ili kupunguza msongamano wa wanafunzi na kutozidi idadi ya 45 kila darasa.

Aidha, aliwataka wananchi kuendelea kuudumisha Muungano ili kupata maendeleo katika nyanja zote.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi

> **Rais Dk. Mwinyi alifafanua kuwa ujenzi wa miundombinu ya skuli ina lengo la kuboresha ili kupunguza msongamano wa wanafunzi na kutozidi idadi ya 45 kila darasa.**

# Majaliwa aonya rushwa kitega uchumi Stendi ya Kange

**Na Mwandishi Wetu, Tanga**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewaonya viongozi wanaogawa maeneo kwenye kitega uchumi kipya cha Dk. Samia Suluhu Hassan Business Centre kilichopo stendi ya Kange, nje kidogo ya Jiji la Tanga, kujiepusha na vitendo vya rushwa.

"Viongozi wote mnaosimamia mchakato wa kuwapata wapangaji wa jengo hili, jiepusheni na vitendo vya rushwa kwa kisingizio cha kutokidhi vigezo. Mkuu wa Mkoa upo hapa, wewe pamoja na watendaji wako, hakikisheni mnachukua hatua stahiki. Fanyeni uhakiki wa vigezo vilivyopo ili kuwezesha wananchi wengi wenye nia kunufaika," alisema.

Alitoa onyo hilo wakati akizungumza na viongozi na wananchi baada ya ya kuweka jiwe la msingi la mradi wa kitega uchumi kilichopo eneo la Kange ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za maadhimisho ya miaka 60 ya Muungano wa Tanzania ambapo kilele chake ni Aprili 26, mwaka huu.

"Kwenye ugawaji wa maeneo kama haya, kuna watu huwa wanadai rushwa, mtu hata biashara yenyewe hajaanza, unataka atoe chochote, mtaji utabakia kweli?," Alihoji na kuwataka wananchi wakati wakifanya maombi yao, wasisite kutoa taarifa iwapo wataombwa rushwa na maafisa wa serikali ili wahusika wakamatwe.

Alisema azma ya serikali ni kuhakikisha kuwa halmashauri zote zinajiendesha na zinajisimamia kwa kutumia mapato yake ya ndani.

"Ili kufanikisha azma hiyo, serikali iliweka mikakati mbalimbali kwa ajili ya kuzigharimia halmashauri ambazo zilibuni miradi ya kimkakati yenye lengo la kutoa huduma bora zaidi na zenye uhakika kwa wananchi. Mradi wa kimkakati wa kitega uchumi wa Jiji la Tanga, ambao leo hii (juzi), nimeuwekea jiwe la msingi, ni moja ya miradi hiyo," alisisitiza.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa

Aidha, alkiwapongeza viongozi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga kwa kutumia kikamilifu fursa za kimapato zilizopo ili kuongeza uwezo wa kujitegemea kwa kubuni na kuandaa mradi huo wa kimkakati wa Jengo la Kitega Uchumi katika Kituo Kikuu cha Mabasi cha Kange.

Wakati huo huo, Waziri Mkuu ametumia fursa hiyo kuwasihi wananchi na viongozi, wafuatilie kwa makini maadhimisho ya miaka 60 ya Muungano na hasa hotuba ya kitaifa ambayo itatolewa kwenye vyombo vya habari na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kesho kuanzia saa 3:00 usiku.

Pia aliwataka wajitokeze kwa wingi na kutoa maoni yao kuhusu Dira ya Taifa waitakayo pindi kamati za kukusanya maoni zikianza kutembelea maeneo yao ili nchi iwe na Dira mpya ya Taifa ya Maendeleo ambayo ni jumuishi na shirikishi.

"Serikali imeanzisha mchakato wa kuandaa Dira mpya ya Taifa ya Maendeleo ambayo inatarajiwa kutoa mwongozo wa mwelekeo wa nchi kwa kipindi cha miaka zaidi ya 25 ijayo. Mheshimiwa Rais alisema vijana ni wengi hivyo washirikishwe kwa wingi. Kama ni afya, semeni mnataka iweje, kama ni biashara, semeni mnataka iweje," alisema na kuongeza:

"Halmashauri zenu na Jiji la Tanga watatoa rasmi siku ya kutoa maoni ili mwende mkatoe maoni yenu. Kama ni michezo au kilimo sema unatamani nini kiwemo. Na je; mawazo yako ni yapi. Tunatamani kuona kila Mtanzania akitoa maoni yake kuhusu Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050."

Kwa upande wake, Mkuu w Mkoa wa Tanga, Dk. Batilda Burian, alisema katika kipindi cha miaka mitatu, zaidi ya Sh. trilioni 2.6 zimepokelewa katika mkoa huo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Alsema kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 159 zimetumika kwenye elimu, ambapo wamejenga shule mpya 77, kwenye maji walipokea Sh. trilioni 1.2 na afya Sh. bilioni 36 ambazo zimetumika kujenga hospitali sita mpya za wilaya na majengo ya dharura.

Mapema, akitoa taarifa ya mradi huo mbele ya Waziri Mkuu, Mkuregenzi wa Jiji la Tanga, Fred Sagamiko, alisema kitega uchumi hicho kimejengwa jirani na stendi kuu, kituo cha daladala, bodaboda na kituo cha maegesho ya malori.

Alisema mradi huo hadi kukamilika kwake utagharimu Sh. bilioni 8.7 na kwamba hadi sasa wameshatumia Sh. bilioni 7.4 kumlipa mkandarasi na Sh. milioni 544.7 ambapo hadi sasa kiasi kilicholipwa ni Sh. bilioni 7.9 ambayo ni sawa na asilimia 90.7 ya gharama za mradi.

Naye, Mhandisi wa Jiji, Issa Rajab Mchezo alisema ndani ya kitega uchumi hicho kutakuwa na ofisi 42 za wakata tiketi za mabasi, eneo la wasafiri kupumzika, maduka, migahawa, vyoo na ukumbi mkubwa wa kufanyia shughuli mbalimbali.

# Wadaiwa Kariakoo kukosa umiliki wa eneo la biashara

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Masoko ya Kariakoo (KMC), limesema halitaruhusu mfanyabiashara mwenye deni la awali, kupata umiliki wa eneo la kufanya biashara katika soko hilo.

Kaimu Meneja Mkuu wa KMC, Sigsibert Valentine, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari juzi.

Aliwataka wafanyabiashara wote wanaodaiwa kulipa madeni yao kabla ya kuomba tena nafasi ya kurejea kwenye maeneo yao ya biashara.

Alisema shirika hilo linadai jumla ya Sh. 497,773,019.26 ambazo ni madeni yaliyolimbikizwa kwa muda mrefu.

"Madeni haya yanapaswa kuwa yamelipwa na wafanyabiashara kabla ya kurejea sokoni ili wapate nafasi ya kusajiliwa kwenye mfumo," alisema.

Alimshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kutoa Sh. bilioni 28.03 zilizotumika kufanikisha mradi wa ujenzi na ukarabati wa Soko la Kariakoo ambao kwa sasa umefikia asilimia 93.

Kuhusu ukusanyaji wa mapato alisema, soko hilo litatumia mfumo wa kielektoniki wa TAUSI kutangaza maeneo ya biashara na kukusanya mapato.



# Nchimbi afunguka mazito uchaguzi

- **Kila chama kipewe nafasi kwa uzoefu wake**
- **CCM ipewe heshima kuendelea kuongoza nchi**
- **Upinzani upewe heshima kuendelea kupinga**

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, amesema pasipo na shaka yoyote, vyama vya upinzani vinafanya kazi nzuri ya upinzani na amewataka wanaCCM kuendelea kuwapa heshima hiyo ya kuendelea kuwa wapinzani.

Amesema kila inapotokea nafasi ya kupiga kura, wakumbuke kuwa wapinzani ni wazuri kuendelea kuwa wapinzani na CCM ni wazuri kuendelea kuongozi nchi.

Aliyasema hayo mjini Mbinga mkoani Ruvuma hivi karibuni wakati akitoa maagizo au maelekezo kwa wanachama wa CCM moja ya njia muhimu za kufanya kupata wagombea mahiri na wenye ari, wakati wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika mwishoni mwa mwaka huu.

Alisema CCM imekuwa madarakani tangu mwaka 1977 na hivyo kuwa Chama chenye uzoefu wa kuongoza na uzoefu wa kuleta maendeleo.

Alisema chama hicho kimethibitisha kwa vitendo kwamba kinajali maendeleo ya Watanzania.

Kwa upande wa vyama ya upinzani, alisema vimekuwepo tangu mwaka 1992 na hivyo kuthibitisha kwa vitendo kwamba vina uwezo mkubwa wa kufanya kazi ya upinzani.

"…kwa hiyo, muendelee kuwapa heshima hiyo ya kuendelea kuwa wapinzani wetu kwa sababu ni kazi wanayoiweza bila shaka yoyote na wanaifanya vizuri mno. Na mkiwapa kazi nyingine, itawashinda," alisema.

Aliwataka kila inapotokea nafasi ya kupiga kura, wakumbuke kwamba wapinzani ni wazuri kuendelea kuwa wapinzani na CCM ni wazuri kuendelea kuongoza nchi.

Akitoa mfano alisema, fundi cherehani mwenye uzoefu wa miaka 15, maana yake ufundi na uzoefu wake hauwezi kupambanishwa na mtu ambaye hana uzoefu.

Aidha, alisema fundi ujenzi wa nyumba mwenye uzoefu wa miaka 40, hawezi kufananishwa na mwingine, lakini kila mtu anakuwa na ujuzi katika eneo ambalo amekuwa akifanyia kazi.

Balozi Dk. Nchimbi alisema CCM wapewe nafasi ya kuendelea kuongoza nchi na kuwaletea Watanzania maendeleo na vyama vya upinzani ambao wameonekana kufanya vizuri sana kazi ya upinzani, wapewe nafasi ya kuendelea kuwa wapinzani.

Katibu Mkuu alihitimisha ziara yake ya kikazi ya siku nne juzi mkoani humo kati ya mikoa sita iliyoanza Aprili 13, mwaka huu ikiwamo Katavi, Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Ruvuma, akiambatana na Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM (NEC) Taifa, Oganaizesheni, Issa Haji Usi Gavu na Katibu wa NEC ya CCM Taifa, Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makalla.



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi



## Samia avutia wazawa kuwekeza nchini

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), limesema katika muda wa miaka mitatu ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan madarakani, kumekuwepo na ongezeko kubwa la wazawa kuwekeza nchini.

Katibu Mtendaji wa NEEC, Being'i Issa, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kongamano la nne la Ushiriki wa Watanzania kwenye uchumi na Uwekezaji litakalofanyika kwa siku mbili Aprili 27 hadi 28 mwaka huu.

Alisema kongamano hilo hufanyika kila baada ya miaka miwili ikiwa ni pamoja kuangalia tathimini ya miaka miwili iliyopita na kuweka dira ya miaka miwili katika uwekezaji kwa wazawa.

Alisema mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko.

# TAKUKURU yafuatilia miradi ya bilioni 61/-

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kinondoni, Dar es Salaam, imefanikiwa kufuatilia utekelezaji miradi sita yenye thamani ya zaidi ya Sh. Bilioni 61 ikiwemo mradi wa ujenzi wa uwanja michezo Mwenge ambao umekamilika kwa asilimia 92.

Hayo yalisemwa na Naibu Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Kinondoni, Elizabeth Mokiwa, wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuhusu utendaji kazi kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia Januari hadi Machi mwaka huu. Alisema miradi hiyo sita ina thamani ya sh 61,910,746,284.42.



Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Kinondoni, Elizabeth Mokiwa

Akizungumzia mradi wa ujenzi wa uwanja wa michezo Mwenge wenye thamani ya Sh. 4,065, 100, 285.25, Mokiwa alisema TAKUKURU inaendelea kufuatilia ili kuhakikisha unakamilika kwa kuzingatia ubora na thamani ya fedha.

Aliutaja mradi mwingine kuwa wa ujenzi wa mtandao wa maji taka na vituo viwili vya kusukuma maji wenye thamani ya Sh. 52, 407, 401, 646. 15 ambao umefika asilimia 60 na unatarajiwa kukamilika Novemba 24 mwaka huu, kwa mujibu wa mkataba.

"Tumefuatilia miradi yote na tumebaini mapungufu machache ambayo wahusika wameshauriwa kurekebisha. Tunaendelea kufuatilia kwa ukaribu hadi miradi itakapokamilika na kuhakikisha inakuwa yenye ubora kwa kuzingatia thamani ya fedha," alisema.

Aidha alisema TAKUKURU imepokea malalamiko 40 yaliyohusu rushwa na kwamba yanaendelea kufanyiwa kazi ili kupatiwa ufumbuzi huku mashauri mawili yakiwa yametolewa maamuzi na Jamhuri (upande wa mashtaka) kushinda.

Alisema wamefungua mashauri mapya matatu na mashauri 19 yanaendelea mahakamani.

Alisema TAKUKURU Mkoa wa Kinondoni inaendelea na mikakati ya kutoa huduma inayowafikia wananchi wote kupitia utekelezaji wa programu ya TAKUKURU – Rafiki ambayo imekuwa na mchango mkubwa kwa kuwafikia wananchi pamoja na wadau mbalimbali ikiwemo wenye jukumu la kusimamia na kutekeleza miradi ya maendeleo.

"Natoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa TAKUKURU na kuwasihi wanapopata taarifa zozote za rushwa watoe taarifa kupitia mitandao yote ya simu kwa kupiga au kutuma ujumbe mfupi kwa namba ya dharura 113- Bure," alisema.

# Waathirika wa mafuriko ya Mlimba wazidi `kupigwa jeki'

**Na Mwandishi Wetu, Kilombero**

MWENYEKITI wa Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM} mkoani Morogoro, Dk. Rose Rwakatare, ametoa msaada wa tani tano za mchele kwa waathirika wa mafuriko wa Jimbo la Mlimba mkoani huku akiwaomba wadau wengine kujitokeza kuwasaidia.

Alikabidhi msaada huo jana kwa Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Dunstan Kyoba katika hafla ambayo iliyofanyika kwenye ofisi ya Mkuu wa Wilaya mkoani Morogoro.

Akizungumza baada ya kukabidhi msaada huo, Dk. Rose alisema amezaliwa Mlimba, hivyo ameguswa mno kuona wananchi wenzake wanaishi maisha ya shida baada ya kukumbwa na mafuriko.



Mwenyekiti wa Wazazi Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Morogoro, Dk. Rose Rwakatare, akimkabidhi Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Dunstan Kyoba, msaada wa tani tano za vyakula kwa waathirika wa mafuriko wa Jimbo la Mlimba mkoani humo katika hafla iliyofanyika jana kwenye Ofisi za Mkuu wa Wilaya. Picha: (Mpigapicha Wetu)

"Mimi ni mzaliwa wa Mlimba, kwa hiyo hapa ni nyumbani kwetu ndiyo maana nimeamua kuja kulia na wanaolia, tufarijiane wakati huu mgumu, sijaja bure nimekuja na tani tano za mchele angalau wapate chakula wakati huu wa shida," alisema Dk. Rose ambaye pia ni Mkurugenzi wa Shule za St Mary's nchini.

Aidha, alimshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kutuma ujumbe kupeleka msaada wa vitu mbalimbali kwa waathirika hao na kuwaomba wadau mbalimbali waendelee kupeleka msaada ya kibinadamu.

"Hata ukiwa na mfuko mmoja wa mchele, unga, mafuta, unakaaribishwa kuja kusaidia Watanzania wenzako kwa sababu wako kwenye hali ngumu sana ya maisha, sisi ni Watanzania na tunajulikana dunia nzima kwa upendo kwa watu wote," alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Kyoba alimshukuru Dk. Rose kwa upendo aliouonesha kwa wakazi wa Mlimba na kuwaomba wadau wengine kuiga mfano huo na kwenda kusaidia vitu vya aina mbalimbali.

Alisema msaada huo umekuja wakati mwafaka kwani wananchi wa maeneo yaliyoathirika na mafuriko, wanahitaji faraja na kushikwa mkono na Watanzania wenzao wakati huu.

"Napenda kutoa wito kwa viongozi wengine na wafanyabiashara, waige mfano wa Dk. Rose Rwakatare waje kusaidia wananchi ambao wako kwenye wakati mgumu wakati huu," alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kilombero, Mohamed Msuya, alimpongeza Dk. Rose kwa msaada alioutoa kwa wananchi hao.

Alisema msaada huo ni wa kuigwa na wa mfano kwa wananchi wa Wilaya ya Kilombero na kwamba bila kujali itikadi za kisiasa, wananchi wanapaswa kuungana wakati huu mgumu kusaidia wenzao.

"Tumpongeze sana Dk. Rose kwa kuwa na maono ya kuwasaidia wananchi wa Kilombero, kutoa ni moyo wala si utajiri kwa sababu kuna watu wana vitu vingi, lakini hawana moyo wa kutoa," alisema na kuongeza:

"Nawaomba sana Watanzania wote bila kujali itikadi, kujitokeza kuwasaidia wananchi wa Jimbo la Mlimba waliopata shida ya mafuriko na tutampa ushirikiano wa kutosha yeyote atakayeleta msaada," alisema na kuongeza

"Dk. Rose Rwakatare, ni mfano wa kuigwa kwa wananchi wa Wilaya ya Kilombero, huyu ana moyo wa kipekee kwa sababu kila linapotokea tatizo, amekuwa msaada mkubwa kwenye Wilaya ya Kilombero."

Alisema baadhi ya watu wanataka kutoa msaada, lakini wanaogopa kutokana na sababu za kisiasa, hivyo amewatoa hofu kwamba wajitokeze kusaidia kwani CCM na Serikali, itawalinda kwa kuwa siasa ni mpaka 2025.

Mkurugenzi wa Mji wa Ifakara, Zahra Michuzi, alimpongeza Dk. Rose kwa msaada alioutoa kwani utawawezesha wananchi waliopata maafa kupata chakula wakati huu ambapo wanajipanga kuanza maisha mapya baada ya janga la mafuriko.

Alisema uongozi wa wilaya hiyo umefarijika mno na msaaada huo ambao aliahidi kuwa watahakikisha unawafikia wahusika kwa wakati mwafaka.

"Nitoe rai kwa wananchi na wadau mbalimbali wa maendeleo wasituchoke bali waendele kutusaidia kwa sababu mahitaji ni mengi kuanzia chakula, dawa, maturubai, tunaomba kila atakayeguswa ajitokeze kusaidia wananchi wetu," alisema.



# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

## HII NI KERO

### Nauli mara mbili

Katika jiji la Dar es Salaam, inapofika jioni ambapo usafiri huwa wa shida, kuna madereva wanaofanya ujanjaujanja ili kuvuna nauli mara mbili. Mara nyingi hukatisha njia au kujenga mazingira ya watu kuwafuata mbali na kuwalipisha mara mbili.

Kwa mfano, madereva wa Temeke - Shule ya Uhuru, wanaposhushia abiria kwenye kona ya Barabara ya Shauri Moyo, na abiria kupandia mahala hapo nyakati za jioni, wanamtoza mara mbili katika eneo lisilofika hata robo kilometa kabla ya kufika kituo cha mwisho. Wizi mtupu!

Ni vyema wamwogope Mungu, na pia abiria wawakomeshe kwa kutofuata magari pale Shauri Moyo ili waje na kupakilia abiria kwenye kituo cha mwisho.



MAONI YA MHARIRI

## Wanaobeza Muungano ni mbilikimo wa kufikiri

Jana, Mbunge wa Viti Maalumu, Mwantumu Dau Haji alisema kwamba Muungano wetu ambao ni wa pekee duniani ni muhimu kutokana manufaa yake.

Mbunge huyo alisema wale wanaobeza Muungano ni watu ambao hawaoni kwa maana kwamba hawana macho na ni mbilikimo (wa kufikiri).

Akichangia Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa mwaka wa fedha 2024/2025 jana Bungeni, Mwantumu alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kudumisha muungano na kuwataka Watanzania wote kudumisha muungano huo.

Alisema changamoto zilizobakia katika Muungano sio kubwa sana na kwamba anaamini kwa kuwa zinafanyiwa kazi zitamalizika moja baada ya nyingine na hata zitakazoendelea kuibuka.

Tunakubaliana na Mbunge huyo kwamba Muungano wetu ambao sasa unafikisha miaka 60 umekuwa na manufaa makubwa na kwakweli anayeubeza ni mvivu wa kufikiri au anategemea maslahi binafsi endapo utavunjika.

Kwa kuwakumbusha tu baadhi ya faida za Muungano wetu ni mafanikio makubwa ambayo yamepatikana ikiwemo kuimarika kwa ulinzi na usalama, maendeleo ya kiuchumi, kukuza tamaduni na lugha ya Kiswahili pamoja na maendeleo ya kisiasa.

Licha kuendelea wa muungano wa kipekee zaidi duniani ambao umedumu kwa miaka 60 uwepo wa sera ya fedha ya pamoja na kuwa na usimamizi wa pamoja wa Benki Kuu ya Tanzania kumesaidia katika kuimarisha uchumi pamoja na kudhibiti mfumuko wa bei kwa pande zote za Muungano.

Muungano umesaifia kukua kwa uwekezaji nchini kutokana na kukuza soko linalochagizwa na Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Sasa hivi Mpemba anaweza kirahisi kabisa kuuza samaki wake Tanzania Bara na mfanyabishara wa Kyela, Mbeya hana vikwazo kwenda kuuza mchele wake Unguja.

Lakini kijamii, mtu wa Musoma anaweza kuoa au kuolewa Zanzibar na kinyume chake na hasa kutokana na kuunganishwa na lugha yetu adhimu ya Kiswahili.

Kuhusu changamoto kwenye Muungano, haziwezi kukosekana kwa sababu Muungano ni sawa na ndoa.

Hayati Rais Ali Hassan Mwinyi ameandika kwenye kitabu cha safari ya maisha yake kwamba kama ilivyo katika ndoa, muungano wa nchi mbili hauwezi kukosa migongano midogo na mikubwa ya hapa na pale.

Mwinyi anasema dawa ya migongano kama hiyo ni ndogo, nayo ni kwa wahusika kuikalia kitako na kuijadili kinagaubaga. Maana, anasema penye nia njema katu hapaharibiki neno. Mwenyezi Mungu hurahisisha mapatano pale wahusika wanapokuwa na nia ya dhati ya kuyatafuta mapatano na maelewano.

Mwinyi anasema hata watu waliwahi kudai Serikali ya Tanganyika ulikuwa mkakati wa kuunda mfumo wa kula tu na wala si uhuru. Maana anasema ni vigumu kuona lipi hasa la msingi ambalo Tanzania Bara inakosa kwenye mfumo wa serikali mbili. Ni vivyo hivyo pia kwa upande wa Zanzibar hakuna wanalokosa.

Ndio maana tunasema wanaobeza muungano ni mbilikimo wa kufikiri.


## Wasiliana nasi

| | |
|---|---|
| **Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000 | **S. L. P:** 15110, Dar es Salaam |
| **Mhariri wa Habari:** +255768411003 | **Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro |
| **Mhariri Michezo:** +255784122020 | **Jengo la:** Aura Mall |
| **Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825 | **Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532 |
| | **Email:** uelekeohabari@gmail.com |


## JICHO LANGU

# Vituo vya kulelea watoto wa watumishi visambae

Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya ilianzisha kituo cha malezi ya watoto kwa ajili ya kutoa uangalizi kwa watoto wa watumishi wa hospitali hiyo wanapokuwa kazini.

Kuanzishwa kituo hicho ni kuwasaidia watumishi wasiokuwa na wafanyakazi wa nyumbani wafanye kazi kwa utulivu na hivyo kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Lakini pia amhatua hiyo inasaidia kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Mpango huo pia unapunguza ruhusa za mara kwa mara kwa watumishi wanawake ambao wamekuwa wakiziomba kwa 'kisingizio' cha kutokuwa na wasaidizi wa kuwaachia watoto wanapokuwa kazini.

Ni kawaida kwenye taasisi baadhi ya watumishi wenye watoto kuchelewa kazini kwa madai hayo hayo ya kuwahudumia watoto, hivyo uwepo wa kituo kama hicho pia unwkomesha 'kisingizio' cha uchelewaji kazini.

Kituo hicho kinawaangalizi wa watoto wenye taaluma hiyo, ikiwa ni pamoja na walimu waliobobea kwenye malezi ya watoto, hivyo watumishi wanapata fursa ya kwenda kuwaona watoto wao kwa ajili ya kuwanyonyesha kwa kuwa wanakuwa katika mazingira ya eneo la kazi na hivyo kuchukua muda mfupi kuwahudumia na kuendelea kuchapa kazi.

Hatua ya hospitali hiyo kuwa na kituo cha aina hii ni muhimu na inasaidia kuongeza ufanisi kazini na ulinzi madhubuti wa watoto kutokana na kulelewa na watalaamu huku pia kituo kikiwa na michezo mbalimbali ya kujenga afya na kukuza ufahamu wa watoto.

> **Hatua ya hospitali hiyo kuwa na kituo cha aina hii ni muhimu na inasaidia kuongeza ufanisi kazini na ulinzi madhubuti wa watoto kutokana na kulelewa na watalaamu huku pia kituo kikiwa na michezo mbalimbali ya kujenga afya na kukuza ufahamu wa watoto.**

Vituo kama hivi, havileti manufaa kwa watumishi ambao hawana mayaya pekee bali hata walio nao kutokana na watoto kulelewa na watalaamu na uhakika wa ulinzi wao dhidi ya unyanyasaji.

Vinaweza kuwa na umuhimu pia kwa watumishi wa kiume hasa kwa kuzingatia mukatadha wa usawa wa kijinsia unaohimiza ushiriki wa namna sawa na wenza wao wa kike katika malezi na makuzi ya watoto.

Ni vyema taasisi mbalimbali za umma na hata za binafsi zikaanzisha uataratibu kama huu kwa sababu mbali na watumishi kuwa na hofu na mustakabali wa watoto wao, lakini ni kweli kabisa kwamba baadhi ya watumishi wamekuwa wakitumia visingizio vya kwenda kuangalia watoto huku wakiwa na mambo yao mengine.

Ni kwa msingi huo, ni vyema hospitali nyingine na taasisi zinazotoa huduma kwa wananchi kama halmashauri mbalimbali, vyombo vya kutoa haki na usimamizi wa sheria, ofisi za wakuu wa mikoa na wilaya na kadhalika na kadhalika zikaanzisha vituo vya aina hii.

Hili ni jambo ambalo linaweza pia kutungiwa sheria na kanuni ili baadhi ya taasisi iwe ni lazima kwao kuwa na vituo vya aina hii, watumishi gani wanapaswa kuvitumia, watoto wa umri gani watalelewa na mengine mfano wa hayo.

# Wizara kushirikiana kuokoa ushoroba Tarangire - Manyara

**Wizara ya Ardhi iko tayari wakati wote kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii kubaini maeneo yote ambayo sisi tunaona ni muhimu yakaachwa kwa manufaa ya Taifa**




Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geofrey Pinda

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

TUME ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii hazina budi kushirikiana kupima na kuweka mipaka ya ushoroba kati ya Hifadhi ya Taifa Manyara na Hifadhi ya Taifa Tarangire ambao uko hatarini kutoweka kutokana na shughuli za kibinadamu zinazoendelea.

Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geofrey Pinda alisema hayo jijini Dodoma jana wakati akifungua kikao cha wadau wa Tume hiyo kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa.

"Wizara ya Ardhi iko tayari wakati wote kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii kubaini maeneo yote ambayo sisi tunaona ni muhimu yakaachwa kwa manufaa ya Taifa," alisema.

Aidha aliitaka Tume hiyo kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii kuchukua hatua za haraka na mapema ili baadaye isije kulazimika kutumia nguvu kuondoa watu katika eneo la ushoroba wa wanayama hao.

Katika hatua nyingine Waziri Pinda amezitaka mamlaka za upangaji nchini ambazo ni Halmashauri kuhakikisha mipango yote iliyoandaliwa kwa kushirikiana na wadau inawasilishwa Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi ili kusajiliwa ili na kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhandisi Anthony Sanga, alisema idadi ya watu katika vijiji imekuwa kiongezeka kwa watani wa asilimia 2.4 kwa mwaka akibainisha kuwa vijijini kuna kaya zaidi ya milioni 8.6 sawa na asilimia 60.3 ya kaya zote nchini.

Alisema ardhi ikipangwa, kupimwa na kumilikishwa itachangia maendeleo ya kiuchumi ikiwemo usalama wa chakula na mtaji muhimu katika kuondoa umasikini.

# DC atamani wanaotaka Muungano uvunjike wachapwe viboko

**Na Mwandishi Wetu, Nachingwea**

MKUU wa Wilaya ya Nachingwea, Mohamed Moyo, amesema kuna watu wanataka Muungano uvunjike kwa maslahi yao, lakini wote wanaotaka hivyo wachapwe viboko ili iwe fundisho kwa wengine.

Moyo alitoa kauli hiyo jana mjini Nachingwea katika mdahalo wa kuelekea siku ya Muungano wa Tanzania.

"Wapo watu wanataka Muungano huu uvunjike kwa masalhi yao, jambo hilo halitakubalika katika jamii yetu, hao wanatakiwa kuchapwa viboko" alisema.

Aidha alisema Muungano wa Tanzania ni nembo kubwa duniani jambo ambalo hadi sasa Tanzania ipo salama baada ya Tanganyika na Zanzibar kuungana na kuwafanya wananchi wote kuwa wa moja.

"Waogopeni kama ukoma wote wanaotaka Muungano uvunjike maana hakuna mwananchi anayetaka kupata ugonjwa huo," alisema Mkuu wa Wilaya Moyo.

**Wapo watu wanataka Muungano huu uvunjike kwa masalhi yao, jambo hilo halitakubalika katika jamii yetu, hao wanatakiwa kuchapwa viboko**

# 'Acheni kuchukua sheria mkononi'

**Na Mwandishi Wetu, Mbozi**

WAKAZI wa Kijiji cha Itewe, Kata ya Itaka, wilayani Mbozi, Mkoa wa Songwe wametakiwa kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi wakati unapotokea uhalifu katika maeneo yao.

Wito huo ulitolewa na Mkuu wa Upelelezi na Makosa ya Jinai Wilaya ya Mbozi, Mrakibu Msaidizi wa Polisi A SP Julius Kishai, wakati akitoa elimu juu ya madhara ya kujichukulia sheria mkononi kijijini hapo jana.

Alisema badala ya kujichukulia sheria mkononi, wanatakiwa kutoa taarifa za uhalifu kwa Jeshi la Polisi ili hatua zaidi za kisheria zichukuliwe haraka.

"Acheni kujichukulia sheria mkononi, toeni taarifa za uhalifu na wahalifu, katika Kituo cha Polisi kilichopo karibu nanyi ikiwa ni pamoja na kuwakamata wahalifu hao na kuwafikisha kituoni au kwa viongozi wa amani ili taratibu za kisheria zichukuliwe dhidi yao," alisema.

# Jopo la Majaji kusikiliza kesi 26 Kigoma



Jaji Mkuu Profesa Ibrahim Juma

**Na Mwandishi Wetu**

KIKAO cha Mahakama ya Rufani kinachoongozwa na Jopo la Majaji Watatu wamepiga kambi mkoani Kigoma kusikiliza kesi 26 katika Mahakama Kuu Kanda ya Kigoma.

Naibu Msajili wa Mahakama ya Rufani, Flora Mtarania, alisema kesi 13 kati ya hizo ni rufaa za makosa ya jinai, sita ni rufaa za kesi za madai, na saba za maombi ya madai.

Alisema jopo linajumuisha Mwenyekiti wa Jopo, Jaji Mwanaisha Kwariko, Zephrine Galeba na Dk. Benhaji Masoud.

"Kesi hizo zitasikilizwa ndani ya wiki tatu katika Mahakama ya Rufani inayoketi chini ya jopo hilo," alisema.

Aidha alisema, jopo hilo la Majaji wa Rufani linakusudia kusikiliza mashauri matatu kwa siku, yaani, kuanzia Aprili 22 hadi Mei 10, mwaka huu watahitimisha kikao hicho.

Alisema, wamepanga kusoma hukumu au maamuzi ya kikao hicho kwa mujibu wa ratiba hiyo ili kuendana na Mpango Mkakati wa Mahakama.

Mapema kabla ya kuanza kwa kikao hicho, Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu, Kanda ya Kigoma, Augustine Rwizile, aliwaongoza watumishi kuwapokea majaji hao waliofika kwa ajili ya kuanza vikao vya Mahakama ya Rufani vilivyopangwa kufanyika katika Kanda hiyo.

# Saratani ya mlango wa kizazi kinara kuwatesa Watanzania

## ● Waziri ahimiza chanjo kwa wasichana

**Na Mwandishi Wetu, Mwanza**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema saratani inayoongoza kutesa Watanzania ni ya mlango wa kizazi, hivyo amewaomba wazazi/walezi kuwapeleka wasichana kupata dozi moja ya chanjo ya HPV ambayo inatosha kumkinga dhidi ya saratani hiyo.

Amesema katika kila wagonjwa 100 wanaougua saratani, 23 ni wa saratani ya mlango wa kizazi.

Aliyasema hayo kwenye uzinduzi wa Maadhimisho ya Dozi moja ya chanjo ya HPV kwa wasichana wenye umri wa miaka tisa hadi 14 iliyozinduliwa katika viwanja vya Furahisha Wilaya ya Ilemela mkoani Mwanza juzi.

"Wataalamu wetu kutoka Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) wametuhakikishia kuwa dozi moja ya chanjo ya HPV, inatosha kumkinga msichana kupata saratani ya mlango wa kizazi," alisema Waziri Ummy na kuongeza:

"Awali dozi zilikuwa zinatolewa mbili, ya kwanza inatolewa leo na baada ya miezi sita inatolewa nyingine hii ilikuwa inasababisha mabinti wengi kutorudi kupata dozi ya pili, sasa hivi tumeamua kutoa dozi moja ya HPV kwa kuwa inatosha kuwakinga wasichana dhidi ya maambukizi ya saratani ya mlango wa kizazi."

Alitaja saratani inayofuata kuwa ni ya mfumo wa chakula ambayo ni asilimia 11, saratani ya matiti asilimia 10.4 na saratani ya tezi dume asilimia 8.9.

Waziri Ummy alitoa wito kwa wazazi na walezi wote nchini, kuhakikisha watoto wanapata chanjo zote wanazopaswa kupata kwa kuwa lengo kubwa la chanjo ni kuwakinga na magonjwa yakiwemo haya ya saratani pamoja na kuwakinga na vifo vinavyoweza kuzuilika na chanjo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, alimhakilishia Mkuu wa Mkoa Mwanza, Saidi Mtanda, kwamba watoto wote wenye umri wa kuanzia miaka tisa hadi 14 watapata chanjo hiyo ili kufikia malengo.



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu

# Wanafunzi waathirika wa mafuriko kuendelea na masomo shule jirani

**Na Mwandishi Wetu, Rufiji**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Profesa Adolf Mkenda, amesema serikali imejipanga kuhakikisha wanafunzi ambao shule zao zimefungwa kutokana na mafuriko nchini, wanaendelea na masomo.

Akizungumza na waathirika wa mafuriko katika Vijiji vya Muhoro na Chumbi B Wilaya ya Rufiji mkoani Pwani, Profesa Mkenda aliwataka wazazi kuwaruhusu watoto wote kwenda shule zilizo karibu na maeneo waliyopo kuendelea na masomo.

"Mafuriko yasiwe sababu ya mtoto yeyote kukosa elimu na kwamba shule zilizo karibu ziendelee kuwapokea wanafunzi kutoka shule zilizoathirika na kufungwa kuendelea na masomo huku serikali ikiendelea na mikakati mingine ya muda mrefu ya kukabiliana na changamoto hiyo," alisema na kuongeza:

"Mwanafunzi yeyote anayepelekwa katika shule iliyo jirani na zile zilizoathirika, apokelewe aendelee na masomo huku taratibu nyingine zikiendelea, ikiwemo uhamisho iwapo mzazi ataridhia abaki hapo. Kikubwa apokelewe kwanza bila vikwazo," alisisitiza Waziri Profesa Mkenda.



Waziri wa Elimu, Profesa Mkenda

# Vijiji 52 Mvomero kunufaika mradi wa LTIP

**Na Mwandishi Wetu**

VIJIJI 52 katika Wilaya ya Mvomero mkoani Morogoro, vinatarajiwa kunufaika na Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi (LTIP) kwa kuandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji.

Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Judith Nguli, alisema hayo juzi wakati wa kujadili utekelezaji wa mradi huo.

Alisema kupitia mradi huu lengo ni kuandaa jumla ya Mipango Shirikishi ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji 52 katika Wilaya ya Mvomero ambapo hadi kufikia sasa tayari mipango 48 imekwishaandaliwa.

"Tarafa nne zilizopo Mvomero zitakazonufaika na mradi huu ni Tarafa ya Mgeta – vijiji 19, Tarafa ya Mvomero – vijiji 11, Tarafa ya Mlali – vijiji 11 na Tarafa ya Turiani – vijiji 11 ambavyo kwa pamoja vitakuwa na jumla ya mipango ya matumizi ya ardhi 52," alisema.

Msimamizi wa Mradi katika Wilaya ya Mvomero, Sambalu Simon, alisema lengo la kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji ni kuimarisha milki za ardhi na matumizi yake, kugawa ardhi na kuboresha matumizi na hifadhi ya ardhi kulingana na mapendekezo na uwezo wa kijiji, kubaini na kutenga maeneo ya umma pamoja na kuimarisha utunzaji wa mazingira kupitia sheria ndogo zinazotungwa kusimamia mpango.

Kwa upande wake, mkazi katika wilaya hiyo Sofia Lucas, alimshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kupeleka mradi huo wilayani kwao, kwa kuwa umewekeza katika kutoa elimu kwa jamii hususani makundi maalumu kama ushiriki wa wanawake katika kumiliki ardhi ili kuwakomboa kiuchumi.



Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Judith Nguli

**"Kwa upande wake, mkazi katika wilaya hiyo Sofia Lucas, alimshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kupeleka mradi huo wilayani kwao, kwa kuwa umewekeza katika kutoa elimu kwa jamii**

Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi unaotekelezwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, umeweka nguvu kubwa katika kutoa elimu kwa wananchi kuanzia ngazi ya kitaifa, wilaya, mtaa/kijiji mpaka kitongoji ikiwa ni pamoja na kuzingatia haki za makundi mbalimbali yakiwemo wakulima, wafugaji, wavuvi, wanawake, vijana, wenye ulemavu sambamba na utoaji wa elimu ya usawa wa jinsia katika umiliki wa ardhi ili kuhakikisha usalama kwa kila kipande cha ardhi kwa Mtanzania.

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

Uelekeo

JARIDA

# Jungu Kuu

| Jumatano Aprili 24-30, 2024 |




Jarida hili haliuzwi



# Msimamo wa Chadema unavyohatarisha Muungano

UK. 12 & 13

# Vijana wafundishwe historia, wajue muungano na faida zake

**Na Mwandishi Wetu**

'Matumaini yangu, yalikuwa kuunganisha nchi hizi za Afrika Mashariki na kuwa muungano mmoja. Kwa upande wa Zanzibar niliongea na Karume, akasema niko tayari, ita watu wa magazeti sasa hivi. Nikamwambia tufanye taratibu na tukafanikiwa."

Hiyo ni kauli ya Mwalimu Julius Nyerere ambaye alikuwa mwanamajumui mkubwa wa Afrika aliyeamini katika muungano.

Akikemea ukabila, umajimbo, udini au ubaguzi wa rangi, mambo ambayo ni sumu ya muungano, Mwalimu pia alipata kusema: "Waingereza na jeuri yao yote wametawala dunia. Wafaransa na jeuri yao yote wametawala dunia. Wajerumani na jeuri yao yote wameipiga Ulaya. Leo wanaungana kuwa taifa moja. Nyinyi Waswahili, vinchi vidogovidogo hivi vya watu ishirini na saba milioni mnazungumza makabila!"

Mwalimu ambaye wakati huo alikuwa pia Mwenyekiti wa Tume ya Kusini (South Commission), alikuwa akizungumzia Umoja wa Ulaya (EU) uliokuwa unaelekea kuzifanya nchi hizo kuwa mithili ya moja, zikiwa na sarafu moja, jeshi moja (NATO), Bunge na mengi ya pamoja lukuki kabla mzizi wa ubaguzi na kujitenga haujamea kwenye myoyo ya Waingereza na kujiondoa kwenye umoja huo.

Kimsingi, Mwalimu kwa kujua umuhimu wa Muungano alikuwa mkali sana juu ya wote waliojaribu kuleta mawazo ya kuvunja Muungano.

Kuna wabunge 55, wakiongozwa na Njelu Kasaka wakati wa uhai wake walijaribu kutikisa Muungano kwa kutaka kuanzisha serikali ya Tanganyika ndani ya Muungano, jambo ambalo lilikuwa lina hatarisha Muungano wetu wa serikali mbili, Mwalimu Nyerere alikuja juu na kukemea vikali.

Lingine lililojiri wakati huo ambalo pia lilikuwa linatikisa Muungano ni pale Zanzibar ilipotaka kujiunga Jumuiya ya Kiislamu (OIC) kivyakevyake, jambo lililokuwa linakwenda kinyume cha katiba ingawa pengine dhamira ilikuwa njema kwamba Zanzibar ilikuwa haijiungi kwa ajili ya dini bali manufaa ya kiuchumi na kijamii ya Jumuiya hiyo.

## WANASIASA KUCHOCHEA CHUKI

Lakini ukiachana na mambo kama hayo, kumekuwa na tatizo la baadhi ya wanasiasa, kuona kama Muungano ni kikwazo cha kutimiza malengo yao ya kisiasa yaliyo nyuma ya pazia.

Hawa wanakuwa na visingizio vingi visivyo na maana kama vile madai kwamba "Watanganyika ndio sasa wanao tuamulia mambo yetu" au madai kwamba "wao ni wachache lakini kwenye nafasi fulanifulani kwa nini tuwe na uwakilishi sawa?" Wanasahau kwamba haya ndio makubaliano ya muungano.

Ndio maana mchambuzi mmoja wa masuala ya siasa na ya kijamii, Habibu Miraji amesema baadhi ya wanasiasa wamekuwa wakijaribu kushawishi wananchi kuchukia Muungano lakini wananchi wenyewe wanaupenda na kimsingi hakuna anayeupinga.

Anasema katika kudhihirisha hilo, Mpemba angetamani akivua samaki wake Pemba akawauze Bara na halikadhalika, Mnyakyusa angetamani akauze viazi vyake Unguja hadi Comoro, hivyo ni dhahiri kuwa wananchi wanautaka Muungano.

## VIJANA KUFAHAMU HISTORIA

Ni kutokana hofu hiyo, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango ametoa wito Watanzania wote hususani vijana kuongeza jitihada katika kufahamu historia ya nchi ili kuhakikisha wanapata uelewa wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Dk. Mpango ametoa wito huo hivi karibuni wakati akifanya mahojiano maalumu na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) kuhusu Miaka 60 ya Muungano.

Makamu wa Rais amesisitiza umuhimu wa kutoa elimu kuhusu Muungano kuanzia ngazi ya shule za msingi. Aidha amesema ni vema kutumia mbinu mbalimbali zinazoendana na vijana katika kutoa elimu hiyo ikiwemo sanaa kama vile muziki na mitandao ya kijamii na kujadili namna ya kujenga na kuimarisha Muungano kwa hoja bila jazba.

## MAFANIKIO YA MUUNGANO

Dk. Mpango amesema katika kipindi cha Miaka 60 ya Muungano, mafanikio makubwa yamepatikana ikiwemo kuimarika kwa ulinzi na usalama, maendeleo ya kiuchumi, kukuza tamaduni na lugha ya Kiswahili pamoja na maendeleo ya kisiasa. Ameongeza kwamba ni Muungano wa kipekee zaidi duniani ambao umedumu kwa miaka 60.

Aidha anasema uwepo wa sera ya fedha ya pamoja na kuwa na usimamizi wa pamoja wa Benki Kuu ya Tanzania kumesaidia katika kuimarisha uchumi pamoja na kudhibiti mfumuko wa bei kwa pande zote za Muungano.

Makamu wa Rais anasema kukua kwa uwekezaji nchini ni kutokana na ukubwa wa soko lililopo linalochagizwa na Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

## MAMBO WANAYOPASWA KUJUA VIJANA

Mbali na kujua faida lukuki za Muunfano, vijana wanapaswa kujua mambo makubwa yaliyosababisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Kuna mambo ya msingi ambayo ndiyo yaliyochagiza kuwepo kwa Muungano. Mambo hayo ni mengi lakini katika makala haya tutaja machache.

Kwanza katika Afrika kulikuwa na vuguvugu kubwa sana la kuhakikisha kwamba nchi zetu hizi zinaungana, tunakuwa wamoja ili Afrika nzima tuwe na nguvu zaidi kwa kuzingatia usemi kwamba "umoja ni nguvu" na utengano ni udhaifu.

Kwa mujibu wa Dk. Mpango, dhana ya kuungana ilikuwa ni moja ya vitu vikubwa sana na viongozi wa wakati ule walikuwa wanajaribu kuona namna ya kuunganisha Afrika nzima.

"Tunakumbuka kwamba (Kwame) Nkrumah kule Ghana na viongozi wenzake wakati ule, Mwalimu (Nyerere), Mzee (Kenneth) Kaunda (wa Zambia) na wengineo (walitaka Afrika kuungana)," anasema Dk. Mpango.

Mpango anaongeza kwamba muungano wetu (hasa) ulikuja kufuatia Mapinduzi matukufu ya Zanzibar ya Januari 12, 1964.

"Kumbe wakati ule kulikuwa bado kuna hofu kule Zanzibar kwamba himaya ya Sultani iliyotimuliwa wanaweza wakajipanga wakarudi tena. Lakini si hivyo tu bali wakasema kama wakija Zanzibar wanaweza kuja (hadi) Tanganyika, hivyo kulikuwa na hofu juu ya usalama wa mataifa haya mawili.

"Kwa miaka mingi, wananchi wetu walikua ni ndugu kuanzia kipindi kile cha utumwa na hata kabla (ya ukoloni). Watu walikuwa na biashara za utumwa, watu wametoka Kigoma na nchi zile za jirani, walikuwa wanapita pale Zanzibar, lakini kulikuwa na msimu wa kuvuna karafuu, wananchi walikuwa wanatoka huku (Bara) wanakwenda kuvuna karafuu... Kadhalika baadhi ya vyakula vilikuwa vinatoka upande wa bara vinakuja Zanzibar. Lakini si hivyo tu, walifika mahali babu zetu wale wanaoana. Hayo ndiyo mambo makubwa aliyosukuma muungano," anasema Dkt. Mpango.

Rais wa Awamu ya Tano, Dk. John Magufuli aliwahi kueleza umuhimu wa vijana wetu kufundishwa kwa umakini mkubwa somo la Historia ya nchi yao na kuwajengea uzalendo kwa nchi yao. Bila shaka wakati umefika kwa hatua hii kuchukuliwa.

Vijana ambao hawafundishwi faida za muungano, historia na namna waasisi wa taifa letu walivyokuwa na uchungu na muungano ni rahisi kurubuniwa na wanasiasa uchwara ili kuuchukia.



## ALI HASSAN MWINYI:

# Muungano kama ndoa, haikosi migongano

**Na Hamisi Kibari**

KATIKA kitabu chake, Mzee Rukhsa: Safari ya Maisha Yangu, Rais wa Awamu ya Pili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Ali Hassan Mwinyi, alizungumzia kuhusu muungano, akisema ni moja maeneo muhimu aliyokuwa akiyangaalia sana kulingana na umuhimu na unyeti wake.

Rais Mwinyi ambaye alifariki dunia Alhamisi, Februari 29, 2024 katika Hospitali ya Mzena, Kijitonyama jijini Dar es Salaam alipokuwa akipatiwa matibabu, katika kitabu hicho ametaja baadhi ya mambo yaliyotokea wakati wa uongozi wake na kugusa muungano na kwamba mengine yalimuudhi Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere lakini mwisho wa siku mambo yalikaa sawa.

Mwinyi katika kitabu chake anamshukuru Mwalimu Nyerere kwa kutoa ushauri mzuri ambao ukitumiwa utazidi kulinda muungano lakini pia anasema kwamba hakuna kitu ambacho Watanganyika wanakosa kwenye muungano wala Wazanzibari.

**Muungano wa nchi mbili huru unafanana na muungano wa ndoa. Lazima kila mmoja wa hao wawili akubali kujipunguzia uhuru wake aliouzowea. Kila mwanandoa hupaswa kati ya watu wawili kumjali mwenzake ili ndoa idumu. Ni lazima kujifunza tabia na hulka za mwenziwe na kuzizingatia.**

### MUUNGANO KAMA NDOA

Katika kitabu chake, Rais Mwinyi anasema ni lazima kukubali pia kuwa muungano wowote ule una changamoto zake na huwezi kutegemea kila siku mambo yawe tambarare.

"Muungano wa nchi mbili huru unafanana na muungano wa ndoa. Lazima kila mmoja wa hao wawili akubali kujipunguzia uhuru wake aliouzowea. Kila mwanandoa hupaswa kati ya watu wawili kumjali mwenzake ili ndoa idumu. Ni lazima kujifunza tabia na hulka za mwenziwe na kuzizingatia," anaandika Mzee Mwinyi.

Anaendelea: "Ili ndoa idumu na kuimarika, kila mmoja lazima ajue na kujali matatizo ya mwenziwe, na wote wawili wajifunze kusikilizana, kuaminiana, kuhurumiana na kuvumiliana. Sifa hizi zinatakiwa pia kwenye muungano wa nchi mbili ili muungano huo udumu na kuimarika mwaka hadi mwaka.

"Na kama ilivyo katika ndoa, muungano wa nchi mbili hauwezi kukosa migongano midogo na mikubwa ya hapa na pale. Dawa ya migongano kama hiyo ni ndogo, nayo ni kwa wahusika kuikalia kitako na kuijadili kinagaubaga. Maana, penye nia njema katu hapaharibiki neno. Mwenyezi Mungu hurahisisha mapatano pale wahusika wanapokuwa na nia ya dhati ya kuyatafuta mapatano na maelewano."

### MUUNGANO NA VYAMA VINGI

Katika kitabu hicho, Mwinyi anaeleza pia jinsi walivyoumiza kichwa wakati wa utawala wake kukubali kwenda kwenye siasa za vyama vingi huku wakihakisha hilo haliwezi kuathiri muungano kutokana na umuhimu na faida zake kwa Watanzania.

"Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama cha Mapinduzi (NEC) iliyoketi Februari 1990, ilizingatia mabadiliko ya kisiasa yaliyokuwa yanatokea duniani wakati huo na kuamua kuwa pengine wakati umefika kwa Tanzania kuwa na mfumo wa vyama vingi vya siasa, lakini kwa namna ambayo haitahatarisha amani, umoja, mshikamano na Muungano wa Tanzania," anaandika Mwinyi.

Anasema kwa kulijua hilo waliamua kupata maoni ya wananchi kuhusu jambo hili kubwa. Anasema ingawa Watanzania wengi walitaka mfumo wa chama kimoja uendelee lakini wakaamua kuingia kwenye mfumo wa vyama vingi huku wakiwa makini hatua hiyo isije ikawa chanzo cha wanasiasa kuleta chokochoko za kuua muungano.

### KUDAI TANGANYIKA NDANI YA MUUNGANO

Mwinyi anaandika kwenye kitabu chake kwamba moja ya jambo lililomsumbua sana alipokuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni madai ya kikundi cha wabunge 55 (maarufu kama G 55) kudai muundo wa muungano wa serikali tatu kwa kufufua serikali ya



Tanganyika na kuunda serikali ya shirikisho.

Anasema ingawa hatimaye idadi ya wabunge waliounga mkono hoja hiyo ilizidi 55, lakini jina la umaarufu la kikundi hicho lilibaki kuwa G55, ikimaanisha kundi la wabunge 55 walioasisi hoja hiyo.

"Jambo hili lilinisumbua sana mwaka 1993, na lilinikumba kwa kushtukiza. Sikulitarajia. Waliolishikia bango walikuwa kundi la wa Bunge lililoongozwa na Mhe. Njelu Kasaka, wakiwemo pia wabunge machachari kama Jenerali Ulimwengu, Matheo Qaresi na wengineo."

Anasema mojawapo ya hoja walioisimamia kwato ilikuwa suala la Zanzibar kujiunga na Jumuiya va Ushirikiano wa Nchi za Kiislamu (Organization of Islamic Conference), ambayo baadaye ilibadili jina na kuwa Organization of Islamic Cooperation (OIC).

"Nilisema wakati ule, na naendelea kuamini, kuwa sababu hasa ya Zanzibar kujiunga haikuwa mambo ya dini bali umaskini tu na matarajio ya misaada. Aliyekuwa Rais wa Zanzibar wakati huo, Mhe. Dkt. Salmin Amour, aliamini kuwa ni kwa maslahi ya Zanzibar kujiunga na OIC kwa matarajio ya misaada mingi kutoka nchi za Kiarabu. Aliona hiyo ni haki ya Zanzibar…" anasema Mwinyi.

Mwinyi anasema suala hilo hilo lilimuudhi sana Mwalimu Nyerere huku akihisi kwamba washauri wake waliogopa kumweleza kuhusu hatari ya jambo hilo.

"Haukuwa woga bali wasaidizi wangu waliogopa kuudhi kundi lolote kati ya wanaodai Tanganyika kwa upande mmoja na Wazanzibari kwa kwa upande mwingine ili wasije kutemwa katika kutafuta uteuzi wa kugombea urais mbele ya safari," anasema.

Mwinyi anasema kwa maoni yake viongozi wanaoingia madarakani si kwa msimamo bali kwa kuyumba kwa kufuata upepo ili kufurahisha watu hawafai.

Anasema ni tukio hili ndilo lilimfanya Mwalimu awe mkali na kufuatilia kwa karibu upatikanaji wa mtu wa kuongoza Serikali ya Awamu ya Tatu ambaye alikuja kuwa Benjamin Mkapa.

Kisha Mwinyi anaandika: "Mnaosoma kitabu hiki mnaweza kuona kuwa Mwalimu Nyerere aliandika kitabu chake cha 'Uongozi Wetu na Hatima ya Taifa' kwa ukali na ghadhabu kubwa kiasi gani. Tena akaenda kukichapisha nje ya nchí, nchini Zimbabwe. Lakini nifikirie mimi ambaye nilikaa naye kitako, faragha, kuyazungumza haya yote yaliyojitokeza katika Muungano wetu.

"Lugha ni kali, lakini hoja zake ni sahihi. Ndio maana nikasema nikitazama nyuma natamani sana tungelishughulikia jambo hili vizuri zaidi kuliko ilivyokuwa na nazidi kumshukuru Mwalimu Nyerere kwa kutushauri vizuri hadi tukalimaliza na hadi leo Muungano wetu unaendelea vema; zinazoitwa kero zake zimepungua sana na chache zilizosalia zinaendelea kushughulikiwa kwa kushirikiana baina ya Serikali zote mbili," anaandikaa Rais Mwinyi.

Mwinyi anaandika kwamba pamoja na kitabu cha Uongozi Wetu na Hatima ya Tanzania Mwalimu Nverere alitunga pia kijitabu kingine, sehemu kubwa ikiwa imeandikwa kwa mfumo wa shairi, alichokiita, Tanzania! Tanzania!

"Hiki alikichapisha nchini mwaka huo huo wa 1993. Ukisoma mashairi yale unaona uchungu mkubwa na kilio cha Mwalimu juu ya Tanzania aliyoiasisi. Unaona pia kuwa hakuwa na uhakika iwapo sisi tulio madarakani tungeweza kuidhibiti hali ile na kuokoa Muungano kutoka katika hatari ya wazi iliyokuwa inatukabili.

"Nikitazama nyuma, naona moto ule wa kudai Serikali ya Tanganyika ulikuwa wa kuunda mfumo wa kula tu na wala si uhuru. Maana ni vigumu kuona lipi hasa la msingi ambalo Tanzania Bara inakosa kwenye mfumo wa serikali mbili. Ni vivyo hivyo pia kwa upande wa Zanzibar," anasema Mwinyi.

"Penye muungano lazima kero zitakuwepo, maana huu ni muungano wa wanadamu, si muungano wa malaika. La muhimu ni kuwa na busara, na kupima. Kwangu mimi (Mwinyi) umoja wetu ukiwa imara ndilo jambo la maana kwa leo na siku za usoni kuliko kuendekeza tofauti na kero ambazo pande mbili zikiamua kwa dhati zinaweza kumalizwa kwa maslahi ya kila upande," anasema Mwinyi.

Nukuu hizo za Mwinyi ni muhimu sana kuzifanyia kazi.




# Msimamo wa Chadema unavyohatarisha Muungano

**Na Hamid Yassin**

IJUMAA ya wiki hii, yaani Aprili 26, 2024, Tanzania itatimiza miaka 60 tangu nchi mbili za Tanganyika na Zanzibar ziungane na kuwa nchi moja.

Ni miaka mingi ambayo tumeshuhudia mengi mazuri na changa moto chache za Muungano huu. Juzi Makamu wa Rais alisema tusiite 'kero' bali 'changamoto' au 'hoja' za muungano.

Lakini kilichonisukuma kuandika makala haya ni jinsi baadhi ya Watanzania wanavyoubeza muungano huu kana kwamba hauna tija yoyote kwa taifa hili.

Kibaya zaidi wanaochagiza kuzungumzia zaidi kasoro za muungano baina ya Tanganyika na Zanzibar kuliko faida zake ni wanasiasa ambao tunawachukulia kama ni kioo cha jamii hususani wale wa kambi ya upinzani.

Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), ndicho kinaongoza kuhoji mamlaka ya nguvu za kikatiba zilizopo upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yaani Zanzibar.

Chadema si tu imekuwa ikihoji nguvu za kikatiba za Zanzibar katika Muungano, bali inazipinga waziwazi; inafanya hivyo kupitia kwenye mikutano ya majukwaa ya kisiasa na iliwahi kufanya hivyo hata katika chombo muhimu cha kutunga sheria za nchi, yaani Bunge.

Kiongozi kinara wa chama hicho anayeongoza kuhoji masuala ya Zanzibar katika Muungano wetu ni Makamu Mwenyekiti wao, Tundu Lissu.

Kila linapojitokeza suala linalohusu Muungano au zinapokaribia sherehe za Muungano, Lissu huibuka na kuwa mbogo kupinga masuala mbalimbali ya upande huo wa pili wa Tanzania.

### HOJA ZA KUOKOTEZA

Hivi sasa Chadema wametangaza ratiba yao mpya ya maandamano na kubadili 'mbinu' za kuyafanya ambapo badala ya kuwa pamoja kila wanapokwenda kama awali, safari hii viongozi wakuu wa chama hicho wamegawana maeneo ya kwenda kufanya hayo maandamano.

Mbali ya kugawana maeneo ya kwenda kuongoza maandamano yao, pia chama hicho kimetangaza kuongeza ajenda za kwenda kuzungumza huko kwenye maandamano yao zikiwemo wanazoita kero za 'Bima ya Afya, Kikokotoo na Muungano'!

Hao ndiyo Chadema, chama cha kucheza na matukiono kwani baada ya sukari kuwa tatizo sana 'wameokoteza' hayo!

Baada ya kuzunguka mikoa kadhaa na ajenda za Katiba mpya na ile hali ngumu ya maisha kwa Watanzania, sasa wameona watumie fursa ya mijadala iliyoibuka kule Bungeni ya mafao ya wastaafu 'Kikokotoo' na Bima ya Afya hususani ule kupitia Mfuko wa NHIF ambayo kimsingi yote imechagizwa na wabunge wa chama tawala, CCM.

### CCM KUFANYIA KAZI KIKOOTOO

Lakini hata CCM imesema imelichukua hilo la kikotoo na kueleza bayana kwamba italifanyia kazi.

Akiwa mkoani Mara, Makamu Mwenyekiti wa CCM, Tanzania Bara, Abudulrahman Kinana alisema CCM imesikia kilio hicho na italifikisha kwenye vikao vya chama hicho na kufanyia kazi.

"Mimi nimesikia sana hii habari ya kikokotoo kinapigiwa kelele nchi nzima, lakini jambo moja ambalo nadhani limetamkwa rasmi hadharani na Katibu Mkuu wa Chama, Ndugu Nchimbi (Dkt. Emmanuel) ni kwamba jambo hili atalifikisha kwa Mwenyekiti wa Chama na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Dk. Samia Suluhu Hassan).

"Kwa maana nyingine atalifikisha jambo hili kwenye vikao husika vya Chama Cha Mapinduzi, litajadiliwa kwa sababu limepigiwa kelele, hatuwezi kujidai hatujui, hatuwezi kujidai hatujasikia na hatuwezi kujidai hatuna habari," amesema.

Ikumbukuwe pia kwamba kule Bungeni mawaziri husika wametolea ufafanuzi mijadala

yote mbele ya wabunge, lakini Chadema kama kawaida yao wameona wazidandie na kuzigeuza fursa mpya kwenye ajenda za maandamano yao wakidhani wanaweza kupata huruma kwa wananchi!

**CHADEMA NA KIKOTOO**

Lakini kwa kuwa mwezi huu pia tunaadhimisha miaka 60 ya Muungano wetu mtukufu baina ya Tanganyika na Zanzibar, kama kawaida yao Chadema kupitia Lissu wamejinasibu kwenda nayo pia kwenye maandamano yao kama ajenda ya kero za muungano!

Kujadili muungano kwa lengo la kuuboresha si jambo baya, lakini ambacho huwa kinaonekana ni kama kupanda mbegu za chuki, watu wauchukie muungano wao, wachukie serikiali moja wapo na mwisho wa siku muungano uvunjike.

Wale wanaofuatilia kwa makini chama hiki watakubaliana na mimi kwamba Chadema wamekuwa wakiliibua mara kwa mara kwa kipindi cha zaidi ya miaka ishirini sasa. Kama nilivyoeleza hapo juu, wamekuwa wakifanya hivyo kwenye viwanja vya mikutano ya hadhara, mitaani na hata kule Bungeni.

Kama Lissu alivyowahi kufanya kwenye kikao cha Bunge la 10 wakati akisoma maoni ya kambi ya upinzani juu ya muswada wa mabadiliko ya katiba ya mwaka 2011,

inawezekana si Lissu binafsi anayepinga baadhi ya nguvu za kikatiba za Zanzibar katika masuala kadhaa yaliyopo kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano, bali ni Chama cha Chadema

Lakini kwa kuwa yeye ndiye alikuwa kinara wa kuzungumzia haya kutokana na nafasi aliyokuwa nayo wakati ule ya Waziri Kivuli wa Sheria na Katiba ndio maana alibebeshwa msalaba ule. Je, hivi sasa kipi kinaendelea kumkera?

Lissu ni msomi aliyebobea katika masuala ya sheria na ni mmoja ya mawakili wazuri tu hapa nchini. Pia kabla ya kugeukia siasa alikuwa mwanaharakati. Lakini kujikita kwake zaidi mara kwa mara katika mambo ya kisiasa, kumemfanya aweke taaluma pembeni na kugeuka kuwa bingwa wa mazingaombwe ya kisiasa.

**KUPINGA UWIANO KATIKA UWAKILISHI**

Chadema imekuwa ikipinga waziwazi masuala ya uwiano wa watu kati ya Tanzania Bara na Zanzibar kwenye vyombo vya maamuzi ya masuala mbalimbali ya Tanzania.

Hoja yake kuu ni kuwa, Zanzibar ni taifa dogo ukilinganisha na Tanzania Bara, haipaswi kuwa na idadi sawa ya watu na upande huu wa pili wa Muungano katika vyombo mbalimbali vya maamuzi kama ile iliyokuwa Tume Huru ya Rais ya kuratibu maoni ya wananchi juu ya Muswada wa Mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2011.

Chadema wanapaswa kuelewa kuwa, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliofanyika Aprili 26 mwaka 1964, ulikuwa ni wa nchi mbili zilizokuwa huru. Yaani Jamhuri ya watu wa Zanzibar na Jamhuri ya Tanganyika.

Mapatano haya ya Muungano yaliyofanywa chini ya waasisi wa mataifa haya mawili, Baba wa Taifa, hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na hayati Abeid Amani Karume, shughuli zake zilitekelezwa katika katiba ya muda ya mwaka 1965 hadi mwaka 1977, ilipopitishwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977.

Katiba hii imekuwa ikifanyiwa mabadiliko mbalimbali kutokana na mahitaji ya wakati husika na matokeo ya mijadala kadhaa ya kile kinachoitwa 'hoja' za Muungano na ndiyo inayotumika hadi hivi sasa.

Mfumo wa Muungano wetu una serikali mbili, ambapo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) ambayo ndiyo yenye Dola 'Sovereignty' inayoshughulikia masuala yote ya Muungano kwa taasisi zinazohusu Muungano na mambo ya Tanganyika ambayo si ya Muungano.

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) ina mamlaka juu ya mambo yasiyo ya Muungano yanayohusu Zanzibar kama ilivyoainishwa katika sehemu ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano na marekebisho yake ya mwaka 1995.

Tunaambiwa kuwa, Chadema ni chama kilichosheheni wasomi, inawezekana ni kweli, lakini hata CCM wamejaa pomoni isipokuwa kina Lissu wanaonekana kiurahisi kutokana na uchache wao ukilinganisha na wale waliojaa kwenye chama tawala na serikali yake.

**WASOMI WA CHADEMA VIPI?**

Hivyo, naamini wasomi hawa wa Chadema wanaelewa fika kuwa, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar imeainisha maeneo 22 ya Muungano ili kuweka mambo bayana kwa pande zote mbili.

Kati ya hayo 22 nitataja machache kwa faida ya wananchi ambao Chadema inadhani ni 'mambumbumbu' wa katiba yetu, hivyo inaweza kuwatumia kama ngazi ya kufanikisha azma zao za kisiasa.

Kubwa la kwanza ni Katiba ya Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; hili ni suala la muungano moja kwa moja.

Pia masuala ya Mambo ya Nchi za Nje, Ulinzi na Usalama, Polisi, Mamlaka juu ya mambo yanayohusika na hali ya hatari, uraia, uhamiaji na la uandikishaji wa vyama vya siasa na mambo mengine yanayohusiana na hayo yameanishwa kama ya Muungano.

Katika mambo hayo 22 yaliyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Zanzibar ina haki sawa na Tanzania Bara bila ya kujali udogo wa nchi yao wala uchache wa watu wake. Haya ndiyo makubaliano yaliyoafikiwa kikatiba tangu Aprili 26 mwaka 1964.

Kwenda kinyume na makubaliano haya kama wanavyotaka Chadema, hakuna tafsiri nyingine zaidi ya kukusudia kuusambaratisha Muungano wetu uliobaki pekee barani Afrika na uliodumu kwa miaka mingi ukilinganisha na nchi nyingi duniani.

**BAADHI YA FAIDA ZA MUUNGANO**

Muungano wa Tanzania ni tunu ya Watanzania wanayostahili kujivunia. Muungano huu una nguvu na unaendelea kushamiri. Katika kipindi cha miaka hii 60 ya Muungano kumekuwa na maendeleo mengi katika sekta za kijamii katika pande zote ambapo wananchi wananufaika katika nyanja mbalimbali.

Wanafunzi toka sehemu zote za Muungano wameweza kupata elimu ya juu katika vyuo mbalimbali vilivyopo hapa nchini bila kubaguliwa. Mfuko wa Maendeleo wa Taifa (TASAF) uliandaa na kutekeleza miradi ya maendeleo katika sehemu zote za Muungano ikiwemo Unguja na Pemba. Je, Chadema wanataka Wazanzibari wapunguziwe huduma hizi kwa sababu ya uchache wao?

Aidha, kuna miradi ya kimkakati kama ule wa Kuondoa Umaskini nchini (NIGP) pande zote za Muungano na mfano mzuri ni ule ujenzi wa soko la Mwanakwerekwe na mradi wa chumvi kule Pemba.

Katika jitihada za kupambana na umasikini, mpaka kufikia mwaka 2007 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikuwa imetekeleza miradi ya kutoa mikopo kwa ajili ya miradi midogomidogo (SELF) kwa sehemu kubwa nchini ambapo jumla ya miradi yenye thamani ya shilingi milioni 380.5 ilitolewa kwa vikundi na mashirika yasiyo ya kiserikali ya Zanzibar pekee. Chadema mpo hapo? Au haikuwa haki kutokana na uchache wao?

Mbali ya hayo, pia Chadema wanatakiwa kuelewa kuwa, hata upatikanaji na ugawaji wa misaada na mikopo toka nje ya Tanzania unaendelea huku kila upande wa Muungano ukipata mgawo wake; kwa mujibu wa makubaliano Zanzibar wanapata asilimia 4.5.

Jambo ambalo limeimarisha umoja na mshikamano wetu, hivyo kudumisha Muungano na uhusiano wa karibu baina ya watu wa pande hizi mbali.

Kitendo cha Chadema wakati ule kupinga wastani uliopangwa wa kura za maoni kati ya Zanzibar na Tanzania Bara juu ya mabadiliko haya ya katiba wanayoyalilia hadi leo kwamba Zanzibar ilipendelewa kwani wao ni wachache, hakikuwa sahihi abadani!

Pia Chadema ililalamika juu ya idadi sawa ya wajumbe saba kutoka kila upande wa Muungano katika Tume ya Rais iliyoratibu maoni ya wananchi ya Mabadiliko ya Muswada wa Katiba, hayakuwa na mashiko zaidi ya kutawaliwa na ubaguzi na dharau kwa Wazanzibari.

Ule haukuwa upendeleo ni haki yao kwa mujibu wa makubaliano ya pande hizi mbili ambapo mawaziri wa wizara husika wa pande zote mbili za Muungano walikaa na wataalamu wao ikiwemo Kamati ya Katiba na Sheria na kupitia kifungu kwa kifungu cha muswada ule uliokuwa unawasilishwa bungeni kwa mara ya pili.

Si masuala haya ya kisiasa tu ambayo Zanzibar imepewa haki sawa na Tanzania Bara. Kwa mfano kifungu cha 147 cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano kinasema kuwa, Mahakama itakuwa na wajumbe sawa wa kuteuliwa kutoka Zanzibar na Tanzania Bara. Sasa itakuwaje mtu ama chama cha siasa kihoji hali hii wakati msingi wake ni katiba yetu?

Kifungu cha 9 (2) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano kinampa Rais mamlaka ya kuhifadhi na kudumisha kuwepo kwa mambo ya Jamhuri ya Muungano, sasa inakuwaje Chadema wanataka kumwondolea rais nguvu hizi za kikatiba kiasi cha kunung'unikia mamlaka yake ya kuteua Tume ya Kuratibu Maoni ya Mabadiliko ya Muswada wa Katiba kama alivyofanya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan mwaka jana?

Hivi sasa vyama vyote vya siasa vinatakiwa kufanya kazi pande zote mbili za Muungano; sasa kwa kauli hizi za viongozi wa Chadema kupinga masuala ya kikatiba dhidi ya Zanzibar, hawaoni kwamba wanajiondolea sifa ya kuwa chama cha siasa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania? Hii pia inatia shaka kama chama hiki siku kiingia madarakani kitadumisha muungano. Dalili zinaonesha watauvunja kutokana na ubaguzi wao.

Chadema wanapaswa kuelewa kuwa, zaidi ya asilimia 84.8 ya Watanzania wamezaliwa baada ya mwaka 1964, hawajui uraia mwingine zaidi ya Utanzania. Hivyo hawawezi kukubali kupoteza hadhi yao hii kwa ubabaishaji wa watu wachache.

***Kwa maoni na ushauri; 0768 888 787 au 0784 122 020.***





# Nafasi yako, ya serikali iko wapi unapolalamikia maisha magumu?

**Na Dk. Felician Kilahama**

Napenda kumshukuru Mungu Mwenyezi, mwingi wa kuturehemu kwa kuniwezesha mara nyingine kuandika makala hii.

Hakika nayafanya haya na mengineyo siyo kwa uwezo wangu mwenyewe bali ni kwa neema yake yeye anayetutia nguvu na kututakia mema binadamu aliowaumba kwa sura na mfano wake.

Makala hii imejikita katika kuangalia nadharia za uchumi. Mtu mmoja mmoja au serikali inahusikaje katika kukua au kuporomoka kwa uchumi na nafasi ya Mwenyezi inaingiaje kwenye ustawi wa mtu.

Nina dhamira njema yenye kutaka kujua uhalisia wa maisha yetu Watanzania walio wengi vijijini na mijini. Je, tuna uelewa mpana kuhusu kukua kwa uchumi na maana yake halisi kwa maisha yetu ya kila siku?

Tanzania Bara ina eneo kubwa kiutawala lililogawanywa katika halmashauri za majiji, manispaa, miji na wilaya jumla yake ni 184 (April, 2024); wilaya 139 na mikoa 26 na majimbo ya uchaguzi 214 (Aprili, 2024).

Mgawanyo huo ni kuhakikisha kuna urahisi wa kuwahudumia wananchi na hivyo kujenga utawala bora na wenye mweleko sahihi wa kuwatumikia na/au kuwahudumia wananchi wake kupitia serikali kuu na serikali za mitaa pamoja na serikali za vijiji na vitongoji husika.

Vilevile, wananchi wanapata huduma mbalimbali kupitia majimbo ya uchaguzi. Kadhalika, kuna vyombo muhimu katika kuimarisha mifumo ya utawala ikiwemo: Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mahakama na taasisi zake.

Lengo kuu ni kuwa na utawala bora (imara) na wenye tija kwa wananchi wake. Kwa mtazamo huo ni wazi kuwa nia ni njema na imefungamanishwa kwenye misingi ya utawala wa kisheria husasni kuwepo Katiba ya Jamhuri ya Muungano Tanzania ambayo ndio Sheria Kuu ya nchi na sheria nyingine, kanuni na miongozo mbalimbali kwa kuzingatia sekta mbalimbali na taasisi/mashirika ya umma na sekta binafsi, kwa faida ya wote. Mwisho wa hayo yote ni kuwa na taifa lenye nguvu kiuchumi na maisha bora kwa wananchi wake.

Sasa turejee kwenye mada husika nia ikiwa ni kutaka kujifunza Waswahili wanasema "aulizaye ataka kujua/kujifunza."

Tangu tupate uhuru wa kujitawala na kufanya maamuzi yetu bila kuingiliwa na taifa lolote ni takribani miaka 63 sasa. Mtu aliyezaliwa wakati tunapata uhuru Disemba 9, 1961 sasa yuko katika kikundi cha wazee wataafu".

Hivyo, ni kipindi kirefu (ingawa siyo sana) lakini toshelezi kuweza kujipima kimaendeleo kwa ujumla wake.

Asili ya andiko hili imetokana na mitazamo ya kijamii kuhusu maendeleo yetu kwa ujumla na kuzingatia shughuli ambazo zimekuwa zikitekelezwa na Serikali tangu tupate uhuru hadi sasa (serikali za awamu sita).

Tunaposema uchumi wa taifa kukua kila mwaka maanake nini? Ni vitu gani vinazingatiwa katika utoaji wa takwimu zanazoashiria ukuaji wa uchumi wa taifa?

Ipo dhana kwamba kiujumla uchumi unaweza kuwa unakua kitaifa lakini hali ya maisha kwa watu wengi ikawa iko chini ya viwango vya kimataifa vinavyoainishwa kwa mtazamo wa mataifa yaliyoendelea sana.

Kwa mfano, kusema watu wa taifa fulani wanaishi chini ya kiwango cha thamani ya 'Dola moja ya Marekani kwa siku hivyo kuitwa masikini. Kwa vipimo vyao, hali hiyo inaashiria kuwa pamoja na uchumi wa taifa husika kukua lakini uhalisia wa maisha ya wananchi wengi yako duni: kifikira, kimapato na kimaslahi.

Hapa Tanzania, uzoefu unaonesha kuwa kumekuwepo na maendeleo ya kiuchumi na kijamii pia hadi taifa likaingizwa kwenye Uchumi wa Kati (middle income state).

Hiyo siyo hatua ndogo, napongeza Serikali zote; ya muungano na ya Zanzibar kuweza kutufikisha hatua hiyo muhimu; ingawa ni kwa vipimo na mitazamo ya walioendelea zaidi yetu.

Ingependeza Watanzania kujua iwapo tumefikia uchumi wa kati kimataifa, je, sasa tunaishi kwa matumizi ya Dola za Marekani ngapi kwa siku au bado tupo kwenye kiwango kilekile cha awali: chini ya dola moja kwa siku?

Kadhalika, kwa kuzingatia taarifa na takwimu zitolewazo na serikali, kupitia vyombo vyake mbalimbali, zinaonesha kumekuwepo na kupiga hatua kimaendeleo.

Hii inatokana na nchi yetu kuwa na siasa safi, uongozi bora, sera zenye mwelekeo sahihi, sheria pamoja na utawala bora. Lakini pia matumizi ya rasilimali zetu (watu, ardhi na maliasili mbalimbali) vimelenga kuinua ubora wa maisha kwa Watanzania wote.

Ukipitia Hotuba ya Waziri Mkuu, ya Makadirio: Mapato na Matumizi kwa kipindi cha 2024/2025; unaweza kupata mwanga na picha kubwa/kamili ya ninachokijadili kwenye makala hii. Mapato ya Serikali kupitia kodi na vyanzo vingine kama utalii na kadhalika; yamekuwa yakiongezeka kila mwaka.

Wawekezaji kwenye sekta mbalimbali wamekuwa wakiongezeka na kuongeza fursa za ajira kwa wananchi. Vilevile, hali ya miundombinu katika ujumla wake, imekuwa ikiimarika kiasi kwamba hali ni tofauti ukilinganisha na miongo mitatu minne iliyopita ikiashiria kuwa kuna kupiga hatua kubwa kitaifa.

Kwa kuzingatia hayo, ndipo sintofahamu ya sipati picha kamili... juu ya uchumi wetu unavyokua kutamanisha kufahamu hali halisi kwa wengi ikoje.

Kwa upande mwingine, ni kutokana na mitazamo ya baadhi yetu pamoja na uchumi kukua bado hali ya maisha kwa wengi vijijini na mijini imegubikwa na malalamiko bado. Ninapopita sehemu mbalimbali mathalani, Dar es Salaam, hasa maeneo yenye mizunguko mikubwa ya watu kama Kariakoo, Ilala Sokoni na viunga vyake, Buguruni, Mbagala Rangi-Tatu, Gongo-la-Mboto; Manzese, Mwenge, Tegeta, Mbezi (Louis), na maeneo ya masoko ya kuuza na kununua bidhaa hasa za chakula; kilio cha wengi unachokisikia ni: hali ngumu ya maisha wakidai mzunguko wa fedha umekuwa mgumu.

Ukiangalia kwenye baadhi ya mitandao ya kijamii, kuna baadhi ya waandikaji wanalalamikia ugumu wa maisha na mlalamikiwa mkubwa ni Serikali. Hakuna hata mmoja anayejitathimini kuona kama hali aliyonayo pengine imesababishwa na uzembe wake, elimu yake duni, weledi wake mdogo au mdau mwingine.

Kuna masuala ya mabadiliko ya tabianchi. Matokeo yake hasi pia yanachangia ugumu wa maisha kwa kuharibu makazi ya watu, kuharibu mazao (chakula/biashara), mifugo, kuharibu miundombinu na kusababisha magonjwa mbalimbali ikiwemo ya mlipuko, wadudu na wanyama hatarishi, hivyo, kusababisha ugumu wa maisha. Je, hao wanaolalamikia serikali kwa kila gumu wanajua wanavyochangia mabadiliko ya tabianchi?

Wakati mwingine yote hayo ni matokeo ya kutokuwa makini katika kujitafutia riziki za kila siku kiasi cha kupelekea hali ya hewa duniani kutokuwa rafiki kwa maisha ya binadamu.

Unapochunguza kujua hasa nini chimbuko la ugumu wa maisha kusema Serikali imesababisha haya yote ni jibu jepesi.

Ukihoji, Je, kuna mahali palipothibitisha kuwa binadamu maisha hayatakuwa na misukosuko kiasi cha kuyamudu maisha kirahisi?

Kimsingi hakuna hali kama hiyo, isipokuwa imeandikwa kwenye misahafu ya imani zetu kuwa binadamu: kwa jasho lake atakula chakula na kuongeza kuwa asiyetaka kufanya kazi asile chakula lakini tunatahadharishwa kuwa tuwe na matumaini mema huku tukipambana ipasavyo mpaka kieleweke.

Hivyo, ukishauri kuwa tufanye kazi kwa bidii na maarifa ili tuweze tujikwamua kiuchumi, kijamii na kimaisha'; hakuna anayeelewa bali wanaona kama unaongezea 'maumivu juu ya majeraha' yao.

Changamoto kubwa ni kwamba wengi tunafanyakazi kimazoea bila kujali kuwa kuna hali ya kupata na/au kukosa. Ukipata mshukuru Mungu na hata kuisifu serikali pia kwa kuweka miundombinu inayosaidia au kurahisishia shughuli zako.

Inatakiwa mambo yakienda mrama tumshukuru Mungu kwa yote na tuendelee kumwomba ili yeye kwa mapenzi yake atusaidie kwa kufanya njia pasipo na njia. Kwa nini tunataka kila wakati tupate na tusipungukiwe; hali ambayo ni ngumu sana wakati hatuchukui hatua stahiki na kusonga mbele kwa kufanya kazi kwa moyo na bidii huku tukimtanguliza Mungu aliye Muweza ya yote na kupitia dua, sala/maombi na kuweka bayana haja za mioyo yetu kwake, huku tukimsihi atusaidie.

Tunapofanya mawasiliano na Mungu tuwe wavumilifu maana Mungu ni msikivu na anatutakia mema; atakapojibu maombi yako shukuru na hata akichelea kujibu jipe moyo huku ukimshuru yeye kwa yote.

***(Inaendelea)***



# Ushauri wa kupewa vitu ni muhimu wanufaika Tasaf

**Na John Ngunge**

WAPO wanaosema kuwa pesa huondoa hasira, huondoa au kupunguza msongo wa mawazo, na mmoja akizipata kamwe macho hayawezi kuwa mekundu kutokana na kukesha kwa mawazo.

Katika kibao chake cha 'Ajali', Bendi ya Muziki ya Msondo Ngoma imejaribu kuelezea kwa namna fulani dhana hii ya mwanaume anapokabiliwa na msongo wa mawazo wa jinsi gani anaweza kutunza familia yake baada ya kupata ajali.

Kwamba hali huwa ni ngumu, mtu huteseka kwa mahangaiko na kujikuta akiwa katika msongo mkubwa wa mawazo.

Lakini wakati mwingine hutokea mtu mwenye shida kubwa ya kiuchumi akapata ngekewa ya fedha ghafla, badala ya kuzigeuza mtaji, akazitumia hovyo mpaka jamii ikabaki inamshangaa!

Makala haya hayalengi kuzungumzia masuala ya ajali bali hali ya familia zinazohangaika na hali duni ya kiuchumi iliyosababisha viongozi wetu kuja na huu Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Kwa mujibu wa Tasaf, awamu ya kwanza ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini ulianza rasmi mwaka 2000 hadi 2005; awamu ya pili ilianza mwaka 2005 hadi 2012.

Awamu ya tatu, kipindi cha kwanza ilianza kutekelezwa mwaka 2013 hadi Desemba, 2019; na kipindi cha pili cha awamu ya tatu kilianza Februari, 2020 hadi Septemba, 2023 ambapo jumla ya kaya maskini 1,100,000 ziliandikishwa na wanufaika kunyanyua hali yao ya kimaisha.

Chini ya mpango huu, walengwa wamekuwa wakipokea ruzuku kila mwezi ambayo baadhi imewanufaisha kwa kuanzisha miradi ya uzalishaji mali kama mashamba, mifugo na shughuli za ujasiriamali ambazo zimewawezesha kuboresha maisha na kujiimarisha kiuchumi.

Hata hivyo, mpango huu unahitaji elimu ya kutosha na endelevu ili kuchagiza wanufaika kuanzisha shughuli za ujasiriamali zitakazowakwamua kiuchumi.

Mbali na elimu ya nadharia, wanufaika wengi wanahitaji elimu ya vitendo katika kufikia azma hiyo.

Wengine wamezitumia kununulia mahitaji ya shule kwa watoto wao, kununulia chakula, kununulia dawa na huduma zingine za afya.

Zamani wanufaika wengi walitumia pesa wanazopata toka Tasaf kuwekeza kwenye elimu ya watoto wao kwa maana ya kuwalipia ada na michango mingine shuleni, lakini baada ya serikali kuja na mpango wa elimu bila malipo, wanufaika wamepata ahueni kwa kuwa pesa hizo sasa wanazitumia kufanya shughuli nyingine za uzalishaji mali ili kuwaingizia kipato.

Zipo taarifa zinazoonesha kwamba wapo wanufaika wa Tasaf walianza na biashara kama ya kufuga kuku tuseme kuku 15, lakini baada ya miaka michache wamekuwa na kuku zaidi ya 100 huku wakiwa pia wameweza kujenga mabanda ya kisasa.

Vivyo hivyo, wapo waliowekeza kwenye mifugo, mashamba, mama lishe na sasa wameshafika mbali huku baadhi wakiwa wametoka kwenye kuishi katika nyumba za udongo na nyasi hadi kujenga nyumba za kisasa zaidi.

Kwa mfano, ukienda kwenye mtandao wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale, unaweza kukutana taarifa za Bi. Pendo Francis Dube, mkazi wa kijiji cha Nyang'holongo ambaye alianza kwa kulima dengu baada ya kupata fedha hizo na kufanikiwa kuvuna gunia nne, kisha akanunua ng'ombe mmoja na alipopata mgao mwingine akakusanya fedha na kuongeza ng'ombe mwingine. Ng'ombe hao wameendelea kuzaliana na kufikia ng'ombe saba. Hii ilikuwa mwaka 2022 na hivyo pengine tunavyoongea mambo yake yameongezeka pia.

Lakini Waswahili wanasema palipo na wengi hapakosi mengi. Kwa bahati mbaya sana, baadhi ya wanufaika wa mfuko huu wamekuwa wakizitumia pesa hizo ndivyo sivyo, tofauti kabisa na malengo ya Tasaf. Wamekuwa wakizitumia kwa kile siku hizi wanachoimba vijana, "kumwagilia moyo".

Ni muhimu sana wanufaika wakumbushwe na kusisitizwa kuacha kutumia pesa wanazopewa 'kumwagilia moyo' au kufanyia anasa zingine ikiwemo kuongeza 'nyumba ndogo'.

Kutumia fedha hizi ndivyo sivyo inarudisha kaya kulekule kwenye hali ya umaskini kuendelea tena na tena licha ya kupokea fedha zinazotolewa na walipa kodi wa Tanzania ili kupitia TASAF zichagize maendeleo ya kaya maskini.

Mpaka sasa kuna baadhi ya waliozitumia pesa hizo kwa mafanikio wameomba waondolewe kwenye orodha ya wanufaika.

Lakini wengine bado hawajafikia kusimama wenyewe kwa miguu yao na hivyo wanaendelea kuwepo kwenye orodha ya wanufaika.

Sasa nini kifanyike? Diwani wa Kata ya Lubonde, wilayani Ludewa, Mkoa wa Njombe, Edgar Mtitu, ametoa mwarobaini wa kuhakikisha kunakuwa na matumizi mazuri ya fedha hizi.

Diwani Mtitu baada ya kuwaelewa vema wananchi wa kata yake, husussan, wanufaika wa mradi huo, aliwafuata Tasaf kuwapa ushauri unaopaswa kuendelezwa kwa wanufaika wa maeneo mengine.

Aliwasilisha serikalini ombi la kutaka wanufaika wa Tasaf katika kata yake wapewe vitu watavyozalisha badala ya fedha. Kwa mazingira ya watu wake yeye alishauri wanufaika wapewe ng'ombe wa maziwa badala ya kukutana na fedha zinazoweza kuwatamanisha au tuseme 'kuwawehusha' na kufanya mambo tofauti.

Mtitu anabainisha kuwa endapo utaratibu huo utasimamiwa vema hakika uchumi wa wanufaika utakua.

Ombi la Mtitu linatokana na kuwepo kwa matumizi mabaya ya fedha wanazopewa baadhi ya wanufaika.

Kwa mfano, alieleza siku wanufaika wanapopewa fedha, baadhi yao hulala nje na wengine hushinda vilabuni wakimwagilia myoyo na kisha hurejea majumbani kwao pesa zinapoisha!

Tumesikia ikisemwa, 'Serikali yetu ni sikivu.' Afisa Mifugo Samwel Nziku na Mtaalamu wa Kilimo Kata, Erick Kapinga wanathibitisha msemo huo kuwa kweli kwa mujibu wa eneo lao la utendaji wa kazi.

Wanasema serikali imeamua kutoa mradi wa ng'ombe wa maziwa kwa wanufaika wa Tasaf, Kata ya Lubonde baada ya Diwani Mtitu kutoa pendekezo hilo.

Chini ya mpango huo, Tasaf imetoa ng'ombe 13 wa maziwa kwa wanufaika wake katika kata hiyo badala ya kuwapa pesa taslimu.

Kata ya Lubonde ina wanufaika 12 chini ya mpango huo, hivyo serikali imetoa majike 12 na dume moja ambalo litatumika na wote.

Wanasema majukumu waliyonayo sasa ni kutoa elimu na matibabu kwa mifugo hiyo.

Diwani Mtitu anasema mbali na kuwainua kiuchumi lakini pia mradi wa ng'ombe wa maziwa utasaidia kukabiliana na tatizo la udumavu na utapiamlo linalosababishwa na kutozingatia lishe.

Anawataka wananchi waliopatiwa msaada wa ng'ombe wa maziwa na serikali kuwatunza vizuri kwa sababu watakapoanza kutoa maziwa itasaidia, mbali na kuwaingizia kipato kwa kuuza maziwa lakini pia kukabiliana na udumavu kwa watoto.

Ni vema elimu ya vitendo kuhusu ufugaji, kilimo au ujasiriamali na utoaji wa vitu mbadala wa fedha vikaendelezwa kama alivyoshauri Diwani Mtitu na ushauri huo kuanza kutekelezwa katika kata yake.

Lakini angalizo hapa ni lazima uwepo ushirikishwaji wa wanufaika wenyewe kuhusu miradi ya ujasiriamali ambayo wangependa kuifanya.

Pengine mwingine mapenzi yake ni kufuga nguruwe, mwingine kufunguliwa genge au kufanya kilimo.

Yule aliyechagua kilimo, kwa mfano, anaweza kusaidiwa kupata shamba lenye rutuba, akapewa mbegu na kukodishiwa kabisa trekta sambamba na kupatiwa mafunzo ya kilimo cha kisasa. Asikutane na fedha.



## Kurunzi

Na Dk. Reubeni Lumbagala | 0620 800 462

# Tunauhitaji sana Muungano kuliko unavyotuhitaji

KESHOKUTWA Aprili 26, 2024 inatimia miaka 60 tangu Tanganyika na Zanzibar ziungane na kuunda Jamhuri Muungano wa Tanzania. Kwa hakika tuna kila sababu ya kujivunia muungano huu ambapo umedumu kwa miaka miaka 60 sasa.

Kwa sheria za kazi na utumishi wa umma, mtu mwenye umri wa miaka 60 anapaswa kustaafu kazi katika utumishi wa umma. Hivyo miaka 60 si haba, ni umri wa mtu mzima ambaye sasa anaingia kwenye uzee.

Waasisi wa muungano huu, Hayati Julius Kambarage Nyerere kwa upande wa Tanganyika na Hayati Abeid Amani Karume kwa upande wa Zanzibar kwa pamoja walikubaliana kuziunganisha nchi zao na kuunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo walichanganya udongo kutoka pande zote kama ishara ya muungano.

Kutokana na raia wa pande zote mbili kuwa ni waafrika, nchi hizi mbili kuwa karibu kijiografia (Geographical closeness), kuongea lugha moja ya Kiswahili, kufanana tamaduni kwa kiasi kikubwa, urafiki wa Hayati Nyerere na Karume, Kufanana itikadi kwa vyama viwili vya Tanganyika African National Union (TANU) kwa upande wa Tanganyika na Afro Shirazi Party (ASP) kwa upande wa Zanzibar na kufanana historia, waasisi hawa waliona ni jambo jema kuungana.

Mchambuzi wa siasa na Diplomasia, Abbas Mwalimu, udugu wa watu wa Tanganyika na wa Zanzibar ulianza tangu karne ya 12, kipindi ambacho hata mwasisi wa Taifa la Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere hakuwa amezaliwa wala Sheikh Abeid Aman Karume.

Anasema udugu huu unaweza kuonekana katika sura ya maeneo ambapo mara nyingi watu huwa na kawaida ya kuhama na majina ya maeneo yao.

"Kwa mfano ukitoka leo ukaenda Msumbiji utakutana na eneo linaitwa Pemba. Lile eneo ukiangalia asili yake utaona Wazanzibari wengi walifanya biashara eneo lile na hata kwenye Muungano ukitoka Dar es Salaam Ukienda Zanzibar utakutana na sehemu inaitwa Magomeni. Hii inaonesha hawa walikuwa ndugu. Kinachowatenga ni jiografia tu. Pia ukienda maeneo ya Mbweni nayo utakutana nako kuna Zanzibar vilevile, Kariakoo ukienda Zanzibar utaikuta na ukienda Pongwe, kuna Pongwe ya Bagamoyo na Pongwe ya Tanga na ukienda Zanzibar kaskazini Unguja unaikuta Pongwe. Sasa unaweza kuona kwa nini majina haya yanashabihiana, hii inakupa picha kuwa hawa walikua ndugu lakini wakagawanywa na sababu za Kijiografia," amefafanua Abas Mwalimu akizungumza katika Studio za Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC).

Mchambuzi huyo anasema nchi mbalimbali zimejaribu kuungana lakini muungano wao ni tofauti na wa Tanzania kwa kuwa Tanzania muungano wake ni baina ya watu na si maeneo na ndio sababu hauitwi Jamhuri ya Muungano ya Tanzania bali Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Neno 'wa' likiwakilisha watu na sio 'ya' ambayo ingewakilisha maeneo.

Manufaa ya muungano wetu yanagusa mambo mengi kuanzia masuala ya kisiasa, kiusalama, kijamii na kiuchumi na hivyo kuwa na kila sababu ya kuendelea kuimarisha muungano huu na kuepukana na chokochoko zote zinazoweka kuhatarisha ustawi wake.

Amani na mshikamano wa kitaifa umeendelea kuimarika sana katika miaka hii 60 ya muungano. Viongozi na wananchi wa pande zote wameendelea kuheshimiana na kulinda na kuhakikisha amani iliyoasisiwa na waasisi wa muungano huu inaendelezwa kikamilifu.

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa pamoja wamekuwa vielelezo katika kuhakikisha amani na mshikamano wa kitaifa unaendelezwa ili wananchi waendelee kunufaika na muungano huu.

Aidha, muungano umeendelea kuwa nyezo muhimu ya kuimarisha udugu wa damu kwa wananchi wa pande zote mbili. Wananchi wote wamekuwa ni ndugu sasa bila kubaguana. Aidha, muungano umesaidia kuchangamana kwa wananchi na hivyo kuoana na kuzaliana. Hii imesaidia sana wananchi kuwa kitu kimoja kupitia kuoana na kuzaliana na kuondoa kabisa suala la ubaguzi. Muungano huu sasa si wa kuchanganya udongo bali kuchanganya damu.



Muungano umesaidia sana kuimarisha suala la ulinzi na usalama. Waasisi wa muungano wetu walidhamiria kusaidiana katika suala la ulinzi na usalama kwani ulinzi na usalama ni kichocheo kikubwa cha maendeleo.

Hivi karibuni akihojiwa na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Makamu wa Rais, Dk. Phillip Mpango aligusia suala la usalama akisema baada Sultani aliyekuwa akitawala Zanzibar kutimuliwa, kulikuwa na tetesi ya kujipanga upya kurejea kuvita na kupiga hadi Tanganyika na hivyo muungano ulikuwa muhimu kwa usalama wa pande zote za muungano.

Ni katika muktadha huo tumeshuhudia miaka 60 yenye mafanikio ya ulinzi na usalama.

Wananchi wameendelea kufanya shughuli zao za uzalishajimali kwa uhuru mkubwa kutokana na kuimarika kwa ulinzi na usalama. Vyombo vya ulinzi na usalama kutoka pande zote vimekuwa vikishirikiana sana kuhakikisha ulinzi na usalama unaendelea kuwepo siku zote.

Muungano pia umekuwa na mafanikio kwa upande wa uchumi kutokana na uhuru uliopo wa raia kutoka pande wote mbili kufanya shughuli za kiuchumi; iwe biashara au ajira ili kuongeza pato lao na nchi kwa ujumla.

Mwananchi kutoka Tanzania bara yuko huru kufanya shughuli za kiuchumi Zanzibar na kinyume chake alimradi afuate taratibu na sheria zinazoongoza kufanya shughuli hizo za kiuchumi na kibiashara.

Muungano vilevile umetoa uhuru kwa wananchi kuwekeza kwenye sekta mbalimbali za kiuchumi, mathalani; kilimo, uvuvi, ufugaji, usafirishaji, madini, nishati na huduma mbalimbali za kijamii.

Uhuru huu umewezesha wananchi kuwekeza katika shughuli hizo na kukuza uchumi. Wananchi pia kupitia muungano wamenufaika kwa kuwa huru kutumia raslimali zinazopatikana kila sehemu ya muungano mathalani ardhi na bahari katika shughuli mbalimbali za kiuchumi wanazozifanya.

Aidha, muungano umesaidia kukuza sekta za utalii, uvuvi na uchumi wa buluu kwa kiwango kikubwa kwa pande zote mbili.

Nihitimishe makala haya kwa kusema, kutokana na manufaa mengi ya muungano, wananchi wa pande zote mbili tuna kila sababu ya kuendelea kudumisha muungano huu kwa nguvu zetu zote. Tunahitajiana sana kuliko wakati wowote katika historia ya nchi zetu hizi mbili.

Juhudi kubwa zinazofanywa na viongozi wa pande zote mbili za kukuza maendeleo zitaendelea kuzaa matunda zaidi endapo tutaendelea kudumisha muungano huu. Kwa hakika tumeshikamana na tumeimarika sana katika miaka 60 ya muungano na ndiyo maana tumepiga hatua kubwa za kimaendeleo ambazo kila mwenye macho anajionea mwenyewe.

***Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.***



Paul Mng'ong'o

KLINIKI YA FIKRA

Simu 0676055444 Email: mngongopaul@yahoo.com



# MAMBO KADHAA KUHUSU FEDHA - 2

Wiki takriban tatu zilizopita tulianza somo hili lenye makusudi ya kuimarisha ufahamu wetu kuhusu fedha. Lakini kwa sababu zilizokuwa nje ya uwezo wetu, tuliishia sehemu ya kwanza na leo tunaendelea na sehemu ya pili. Ni muhimu kufahamu mambo haya kwa undani kama una malengo ya kukua kifedha.

Mambo haya ninayokuletea hapa ni sahihi kabisa na yamehakikiwa na kutolewa pia na mwongozo wa nyenzo ya kufundishia elimu ya fedha uliotolewa na Wizara ya Fedha. Karibu tuendelee na safu hii sehemu ya pili kwa faida yako na ustawi wa jamii yetu.

**KABLA YA KUINGIA KWENYE MKOPO, HAKIKISHA MAMBO YA MSINGI YAFUATAYO: -**

**1 MKOPO NI NINI?**

Mkopo ni fedha iliyotolewa na mtu binafsi/taasisi za fedha kwa mtu au taasisi ambayo ni lazima irejeshwe katika muda uliopangwa pamoja na riba na gharama nyingine zinazoambatana na mkopo huo kama vile gharama za taratibu za kupata mkopo na bima.

**2 DHAMANA YA MIKOPO**

Dhamana ni kitu ambacho mkopaji anamiliki (mfano sehemu ya ardhi, gari, nyumba, mwajiri nk.) na anaweka kama dhamana kipindi anapokopa na mkopeshaji anaweza kuchukua dhamana hiyo kama mkopaji atashindwa kulipa mkopo husika.

Baadhi ya wakopeshaji wanakubali mtu mwingine kuwa mdhamini na ikiwa mkopaji atashindwa kulipa mkopo, mdhamini atalazimika kulipa mkopo huo kwa ajili yake. Hivyo, ni muhimu kwa mdhamini kuwa makini kabla ya kudhamini mikopo ya watu.

Pamoja na kutoa ushahidi wa dhamana mkopaji anaweza kutoa uthibitisho wa mzunguko wake wa fedha (Cash Floor) ya shughuli zake za biashara kwa mkopeshaji. Hii itampa mkopeshaji uelewa wa uwezo wa mkopaji kulipa mkopo na kufanya maamuzi ya kumpa au kutompa kiasi cha mkopo anachostahili.

**3 GHARAMA ZA MKOPO**

Mkopaji anapaswa kufahamu gharama za mkopo na kuziafiki kabla ya kuchukua mkopo. Gharama hizo ni pamoja na: riba na ada nyingine zilizoainishwa katika mkataba wa mkopo. Kabla ya kuchukua mkopo, muulize mkopeshaji kuhusu jumla ya kiasi ambacho unapaswa kulipa katika kipindi chote cha mkopo. Ni wajibu wa mkopeshaji kumfahamisha mkopaji jumla ya gharama zote zinazohusiana na mkopo husika.

Hii ni tahadhari muhimu sababu wakopaji wengi wanaangalia tu kile wanachokopa na hawazingatii gharama za mkopo huo na wengi hujikuta wamejiingiza kwenye mikopo isiyolipika sababu ya ukubwa wa gharama za mkopo.

**4 RIBA**

Riba ni kiwango cha gharama ya mkopo ambacho hulipwa kwa mtu au taasisi ya fedha inayokopesha. Riba hukokotolewa kutoka kwenye kiwango cha mkopo uliotolewa, ambapo kwa kawaida huwa ni asilimia ya kiasi cha mkopo kwa kipindi husika.

Sasa ni vizuri upate ufafanuzi wa kutosha na kama huelewi sana mambo ya asilimia, omba mchanganuo wa deni zima na mchanganuo wa marejesho kuanzia mwezi wa kwanza hadi wa mwisho.

Hii itakupa kujua kila mwezi utatakiwa kurejesha shilingi ngapi na hivyo kwa miezi yote utakuwa umelipa shilingi ngapi? Ufahamu huu ndiyo utakuwezesha kujua kama unaweza au huwezi.

**Aina za Riba**

Riba inaweza kuwa isiyobadilika (Flat interest Rate) au inayobadilika (Reducing balance interest rate).

Riba inayobadilika hutolewa kulingana na kiasi cha mkopo ambacho hakijarejeshwa. Riba isiyobadilika kiwango chake huwa hakibadiliki wakati wote wa kurejesha mkopo. Kutambua aina za riba kunakuwezesha kupanga kwa usahihi namna ya kurejesha mkopo.

**Adhabu za Kutolipa / Kuchelewa kurejesha Mkopo**

Unajua ni adhabu gani utapata ikiwa hutolipa mkopo wako kwa muda?

Mkopaji anatakiwa kufahamu adhabu au faini atakazotozwa ikiwa atashindwa kurejesha mkopo kwa wakati kupitia mkataba au sera ya mkopo ya taasisi. Usipolijua hili unaweza kukutana na tatizo kubwa ambalo hukulitarajia.

**5 NAMNA YA KUPATA MKOPO WA GHARAMA NAFUU**

Wakati unataka kuchukua mkopo, linganisha gharama za mikopo inayotolewa kutoka taasisi mbalimbali za fedha kwa kuzingatia viwango vya riba, muda wa kurejesha mkopo, tozo na adhabu za kushindwa kurejesha mkopo kwa wakati.

Kukopa kwa mkopeshaji mwenye gharama nafuu za mkopo kutamwezesha mkopaji kulipa mkopo kwa wakati, hivyo ni muhimu mkopaji kufanya utafiti wa gharama na masharti ya mkopo kabla ya kukopa. Ni wajibu wa mkopeshaji kutoa taarifa zote zinazohitajika kwa mkopaji ili aweze kufanya maamuzi sahihi.

Kama ungependa kupata ushauri au usimamizi wa karibu katika kuishi mwongozo huu, (Unaweza kuwa Taasisi, kikundi, kanisa, umoja, NGO au mtu binafsi), karibu sana tutashirikiana nawe kwa neema na msaada wa Mungu. Karibu uwasiliane nasi kwa namba 0676055444 au barua pepe mngongopaul@yahoo.com

***Wework Consult - Your Partner in Growth***

***ITAENDELEA WIKI IJAYO.***

# Jinsi chumvi inavyoathiri mwili na kusababisha magonjwa



WATU hutumia chumvi tangu mwanzo wa ustaarabu wa kusindika, kuhifadhi na kuboresha chakula.

Katika Roma ya kale, chumvi ilikuwa muhimu mno kufanya biashara kiasi kwamba askari walilipwa mshahara wao, kwa mfano, kwa chumvi.

Thamani ya chumvi ilikuwa kwa kiasi fulani kama kuhifadhi chakula, kudhibiti vijidudu visivyohitajika na kuruhusu vile vinavyohitajika kukua.

Ni uwezo huo wa ajabu wa kudhibiti ukuaji wa bakteria ambao huenda ulisaidia kukuza vyakula vilivyochacha kuanzia sauerkraut hadi salami, kutoka kwa zeituni hadi mkate, kutoka jibini hadi kimchi (mboga zilizotiwa chumvi na chachu).

Hata hivyo, upo ushahidi unaoongezeka kwamba chumvi nyingi (hasa kloridi ya sodiamu inayoongezwa ili kuhifadhi na kuongeza ladha ya vyakula vingi vilivyochakatwa), inawafanya watu kuwa wagonjwa.

Inaweza kusababisha shinikizo la damu na kuchangia mashambulizi ya moyo na kiharusi. Pia inahusishwa na ongezeko la hatari ya kupata saratani ya tumbo na koloni, ugonjwa wa Ménière (tatizo la sikio la ndani ambalo linaweza kusababisha kizunguzungu), mifupa na uzito uliokithiri.

## SHINIKIZO LA DAMU

Jukumu la sodiamu katika shinikizo la damu na ugonjwa wa moyo ni kwa kiasi kikubwa kwa sababu inadhibiti kiasi cha maji ndani ya mishipa ya damu.

Kwa maneno rahisi, zaidi ya sodiamu katika damu, maji zaidi huvutia ndani ya mishipa ya damu.

Hii husababisha kuongezeka kwa shinikizo la damu na hatari ya kutokea mshtuko wa moyo na kiharusi.

Chumvi husababisha kupungua kwa vijidudu vyenye afya na metaboli muhimu wanazozalisha kutoka kwenye nyuzi.

Metaboli hizi hupunguza uvimbe kwenye mishipa ya damu na kuifanya itulie, ambayo husaidia kupunguza shinikizo la damu.

Isipokuwa kwa viumbe fulani ambavyo hustawi katika chumvi, inayoitwa halophiles, viwango vya juu vya chumvi vinaweza sumu karibu na vijidudu vyoyovyote, hata wale ambao mwili wako unavihitaji.

Ndiyo maana watu kwa muda mrefu wamekuwa wakitumia chumvi kuhifadhi chakula na kuwaepusha na bakteria wasiohitajika.

Lakini mlo wa kisasa mara nyingi huwa na sodiamu nyingi. Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), matumizi ya kiafya ni chini ya miligramu 2,000 kwa siku kwa mtu mzima wa wastani.

Wastani wa ulaji kimataifa wa miligramu 4,310 za sodiamu kuna uwezekano umeongeza kiwango cha chumvi kwenye utumbo juu ya viwango vya afya.

## CHUMVI KATIKA UZITO MKUBWA

Sodiamu inahusishwa na matokeo mengine ya afya kando na shinikizo la damu na microbiome yako inaweza kuwa na jukumu hapa pia.

Lishe ya juu ya sodiamu na viwango vya juu vya sodiamu kwenye kinyesi, vinahusishwa kwa kiasi kikubwa na matatizo ya kimetaboliki, ikiwa ni pamoja na sukari ya juu ya damu, ugonjwa wa ini na kuongezeka kwa uzito.

Uchunguzi mmoja ulikadiria kuwa kwa kila gramu ya ongezeko la kila siku la sodiamu ya lishe, kuna hatari ya kuongezeka kwa asilimia 15 ya uzito.

Utafiti wa kawaida wa lishe kutoka Taasisi za Kitaifa za Afya za Marekani, uligundua kuwa wale waliofuata lishe ya vyakula vilivyosindikwa kwa wiki mbili, walitumia kalori 500 zaidi na walikuwa na uzito wa kilo moja zaidi ikilinganishwa na wale waliofuata lishe ndogo.

Moja ya tofauti kubwa kati ya milo hii miwili ilikuwa matumizi ya ziada ya gramu 1.2 za sodiamu na vyakula vilivyochakatwa zaidi.

Moja ya maelezo ni kwa nini kuongezeka kwa chumvi kunaweza kusababisha kupata uzito licha ya kutokuwa na kalori ni kwamba sodiamu huongeza matamanio.

## MATAIFA YANAYOPUNGUZA MATUMIZI YA CHUMVI

Wakati nchi nyingi zinatekeleza mipango ya kitaifa ya kupunguza chumvi, matumizi ya sodiamu katika sehemu nyingi za dunia, yanaendelea kuongezeka.

Kupunguza chumvi ya lishe nchini Marekani hasa kunaendelea kudorora, wakati nchi nyingi za Ulaya zimeanza kuona faida kama vile shinikizo la damu na vifo vichache vinavyotokana na ugonjwa wa moyo kupitia mipango kama vile kuweka lebo ya chumvi kwenye vifurushi, urekebishaji wa chakula ili kupunguza chumvi.

Ulinganisho wa data ya lishe kwa bidhaa za chakula cha haraka kati ya nchi unaonesha tofauti kubwa.

Kwa mfano, kuku wa McDonald's ni chumvi zaidi nchini Marekani na hata Coca-Cola ya Marekani ina chumvi, kiungo ambacho hakipo katika nchi nyingine.

Sekta ya chumvi nchini Marekani inaweza kuwa na jukumu katika suala hili.

Alisisitiza kuepuka kanuni za serikali kuhusu chumvi katika miaka ya 2010, tofauti na vile sekta ya tumbaku ilifanya na sigara katika miaka ya 1980.

## VYAKULA VYENYE CHUMVI VINAUZWA VIZURI.

Mojawapo ya sauti kuu za tasnia ya chumvi kwa miaka mingi, Taasisi ya Chumvi ambayo sasa haifanyi kazi, inaweza kuwa imechanganya ujumbe wa afya ya umma kuhusu umuhimu wa kupunguza chumvi kwa kusisitiza hali ambazo hazijazoeleka sana ambapo kizuizi cha chumvi kinaweza kuwa hatari.

Lakini kuna ushahidi unaoongezeka wa haja ya kupunguza chumvi katika chakula, na taasisi zinajibu.

Mwaka 2021, Idara ya Kilimo ya Marekani, ilitoa muongozo mpya ikitoa wito wa kupunguzwa kwa hiari polepole kwa chumvi katika vyakula vilivyotayarishwa kibiashara na kusindika.

Taasisi ya Chumvi ilivunjwa mwaka wa 2019. Mashirika mengine, kama vile Taasisi ya Vyakula Vilivyohifadhiwa Marekani na wasambazaji wakuu wa viambato, kama vile Cargill, wanakubali kupunguza chumvi kwenye lishe.

## UWIANO SAWA

Unawezaje kulisha vijidudu vya utumbo wako vizuri ukizingatia ulaji wako wa chumvi?

Anza kwa kupunguza ulaji wako wa vyakula vilivyochakatwa sana : nyama zenye chumvi nyingi (kama vile chakula cha haraka na nyama iliyokaushwa), chipsi zenye chumvi na vitafunwa vyenye chumvi nyingi (kama vile soda, vitoweo na mikate).

Hivi sasa, hadi asilimia 70 ya chumvi katika lishe ya Marekani, hutumiwa kutoka kwenye vyakula vilivyosindikwa.

Badala yake, zingatia vyakula ambavyo havijaongezwa sodiamu na sukari na potasiamu na nyuzinyuzi nyingi, kama vile vyakula vya mimea ambavyo havijasindikwa: maharage, karanga, mbegu, nafaka, matunda na mboga.

Vyakula vilivyochachushwa, ilhali kwa kawaida, huwa na sodiamu nyingi, vinaweza pia kuwa chaguo bora kiafya.

Hatimaye, fikiria uwiano wa sodiamu na potasiamu katika chakula. Ingawa sodiamu husaidia kuweka maji katika mishipa ya damu, potasiamu husaidia kuweka maji katika seli. Sodiamu ya chakula hutumiwa vyema kwa uwiano wa usawa.

*BBC.*

## Biden kusambaza msaada mpya wa kijeshi Ukraine

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS Joe Biden wa Marekani, amemwambia Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky kuwa atachukua hatua haraka kutuma msaada mpya wa kijeshi wa Ukraine, baada ya wabunge wa Marekani kupitisha kifurushi cha msaada cha Dola bilioni 61.

Baraza la Wawakilishi liliidhinisha muswada huo Jumamosi niliyopita baada ya miezi kadhaa ya msukosuko wa kisiasa katika bunge hilo.

Rais Biden aliahidi msaada muhimu kwa Kyiv ikiwa ni pamoja na ulinzi zaidi wa anga ikiwa maseneta wataidhinisha muswada huo kama ilivyotarajiwa jana Jumanne.

Uhakikisho huo unatokea wakati mashambulio ya Urusi yakiharibu mnara wa Tv huko Kharkiv.

Picha zilionyesha mnara huo mwekundu na mweupe, ukiporomoka sekunde chache baada ya makombora ya Urusi kuushambulia juzi alasiri katika mji wa Mashariki mwa Ukraine, ulio umbali wa kilomita 30 kutoka mpaka wa Urusi.

Maafisa wa eneo hilo walisema hakukuwa na majeruhi katika shambulio hilo, huku Gavana wa eneo hilo, Oleg Syniehubov akiandika kwenye mitandao ya kijamii kwamba wafanyakazi walikuwa kwenye makazi wakati shambulizi hilo linatokea.

Syniehubov aliongeza kuwa shambulio hilo limetatiza utangazaji wa televisheni katika eneo hilo.

Kharkiv imekuwa ikilengwa katika mashambulio ya angani yasiyokoma na vikosi vya Urusi katika wiki za hivi karibuni.

Katika ujumbe mtandaoni baada ya shambulio hilo, Rais Zelensky aliandika kwamba ilikuwa "nia ya wazi ya Urusi kufanya mji huo usiwe na watu."

Aliongeza: "Alikuwa amemjulisha Rais Biden kuhusu shambulizi hilo, ambalo lilifanyika kabla ya kuzungumza kwa njia ya simu siku ya Jumatatu." BBC.



# Watu 10 wafa helikopta za Jeshi zikigongana angani

**KUALA LUMPUR, Malaysia**

WATU wamefariki dunia baada ya helikopta mbili za Jeshi la Wanamaji kugongana angani wakati wa mazoezi ya kijeshi ya gwaride la Wanamaji wa Kifalme Malaysia.

Moja ya ndege hizo ilinasa propela ya ndege nyingine kabla ya zote kuanguka chini, kulingana na video iliyoonyeshwa na vyombo vya habari vya ndani.

Tukio hilo lilitokea saa 09:30 kwa saa za huko katika mji wa Malaysia wa Lumut ambao ni kitovu cha Kambi ya Jeshi la Wanamaji.

Hakuna manusura walioonekana.

"Waathiriwa wote walithibitishwa kuwa wamefariki dunia kwenye eneo la tukio huku mabaki yakipelekwa katika Hospitali ya Jeshi ya Lumut kwa utambulisho," Jeshi la Wanamaji la Kifalme la Malaysia lilisema.

Imeongeza kuwa itaunda kamati kuchunguza chanzo cha tukio hilo.

Moja ya helikopta, HOM M503-3 ikiwa na watu saba, inaaminika kuanguka kwenye njia ya ndege.

Nyingine, Fennec M502-6 iliyokuwa imebeba waathiriwa wengine watatu, ilianguka kwenye kidimbwi cha kuogelea kilichokuwa karibu.

Idara ya Zimamoto na Uokoaji ya jimbo hilo, ilisema iliarifiwa kuhusu tukio hilo saa 09:50 kwa saa za ndani BBC.



# Kesi ya ANC dhidi ya chama cha MK yatupiliwa mbali

**JOHANNESBURG, A. Kusini**

CHAMA Tawala nchini Afrika Kusini cha African National Congress (ANC), kimeshindwa katika kesi ya pili mahakamani dhidi ya chama kipya cha upinzani kinachoongozwa na aliyekuwa Rais, Jacob Zuma.

Hukumu hiyo ilitolewa na Mahakama Kuu ya KwaZulu - Natal juzi.

Jaji mmoja katika Mahakama Kuu ya KwaZulu-Natal katika Jiji la Mashariki la Durban, alitupilia mbali kesi ya ANC inayodai ukiukaji wa hakimiliki dhidi ya chama cha MK Party kwa kutumia jina na nembo ambayo ANC inadai umiliki wake.

UMKHONTO WESIZWE
MK

Chama cha MK kiliundwa mwishoni mwa mwaka jana na kilipewa umuhimu zaidi kabla ya uchaguzi wa kitaifa Mei, mwaka huu.

MK inachukua jina lake kamili uMkhonto weSizwe kutoka kwa mrengo wa kijeshi uliovunjwa sasa ulioanzishwa na ANC na Nelson Mandela, katika miaka ya 1960.

Nembo ya Chama cha MK inayoonyesha mtu aliyeshika mkuki na ngao, ni sawa na nembo ya mrengo wa kijeshi wa zamani.

Ombi la ANC la malipo kwa njia ya mrabaha au fidia kutoka kwa MK, lilikataliwa.

VOA.

**VITA VYA ISRAEL, GAZA:**

# Wanafunzi vyuo vikuu Marekani waandamana

**WASHINGTON, Marekani**

MAANDAMANO ya kupinga vita huko Gaza, yameenea kutoka Columbia na Yale hadi vyuo vikuu vingine nchini Marekani huku maafisa wakihangaika kukabiliana nayo.

Juzi usiku, polisi walitawanya maandamano katika Chuo Kikuu cha New York na kukamata watu kadhaa.

Wanafunzi wengi walikamatwa huko Yale mapema siku hiyo Columbia ilipositisha masomo ya ana kwa ana darasani.

Maandamano kama hayo yameibuka huko Berkeley, MIT na vyuo vingine kote nchini humo.

Maandamano na mijadala mikali kuhusu vita vya Israel na Gaza na uhuru wa kujieleza vimetikisa vyuo vikuu vya Marekani tangu kutokea kwa shambulio la Hamas dhidi ya Israel Oktoba 7, mwaka jana.

Takriban Waisrael na raia wa wageni 1,200, waliuawa na wengine 253 walipelekwa Gaza kama mateka, kulingana na hesabu za Israel.

Israel ilijibu kwa kuanzisha vita vyake vikali zaidi kuwahi kutokea huko Gaza kwa malengo ya kuwaangamiza Hamas na kuwakomboa mateka.


Zaidi ya Wapalestina 34,000 huko Gaza, wengi wao wakiwa watoto na wanawake, wameuawa katika mzozo huo, Wizara ya Afya ya eneo hilo inayoendeshwa na Hamas, inasema.

Nchini Marekani, wanafunzi wa pande zote mbili wanasema kumekuwa na ongezeko la matukio ya chuki dhidi ya Wayahudi na Uislamu.

Alipoulizwa kuhusu maandamano ya chuo hicho juzi, Rais Joe Biden wa Marekani, alisema alilaani "maandamano ya chuki dhidi ya Wayahudi" pamoja na "wale ambao hawaelewi kinachoendelea na Wapalestina." BBC.







# Xabi Alonso hatasahaulika daima Leverkusen

**Na Valensi Mbaga**

KIKOSI cha Xabi Alonso cha Bayern Leverkusen ni miongoni mwa timu zinazozungumzwa zaidi duniani kwa sasa kwani hivi karibuni walinyanyua taji la Bundesliga kwa mara ya kwanza katika historia ya klabu hiyo.

Wamefanikiwa kufanya hivyo huku wakiwa hawajafungwa kwenye ligi baada ya kucheza raundi 31 msimu huu.

Kuiondoa Bayern Munich katika mbio za ubingwa ambao walikuwa washindi wa Bundesliga kwa misimu 11 mfululizo iliyopita na timu kubwa na wababe wa soka nchini humo kwa miongo kadhaa, ni jambo la ajabu.

Leverkusen imecheza michezo 43 bila kupoteza mechi katika mashindano yote msimu huu na sasa imeshinda kombe lake la kwanza tangu 1993.

Tukio hilo muhimu liliibua matukio ya shangwe ndani ya uwanja uliokuwa umejaa watu wa BayArena, huku mashabiki wakikimbilia uwanjani kusherehekea na wachezaji. Alonso aliongoza sherehe hizo.

"Tulitaka kucheza michezo kwa mtazamo mzuri msimu huu na wachezaji walianza kufanya kazi pamoja haraka. Baada ya mechi chache za kwanza, tuliona timu hii inaweza kucheza soka nzuri sana," Alonso alisema

"Lakini kufanikisha hili kwa njia kama hiyo ilikuwa utendaji wa hali ya juu. Hatimaye, ni heshima kusema kwamba Leverkusen ni mabingwa. Inastahili kabisa kwa timu, mashabiki na klabu."




Mbio za ushindi za Leverkusen kwenye ligi zilitoka nje ya dira, huku klabu ikiwa katika hali mbaya wakati Alonso alipojiunga mnamo Oktoba 2022.

Ilikuwa ya pili chini ya Bundesliga na katika hali mbaya. Lakini katika kipindi cha miezi 18, Alonso amefanya mapinduzi makubwa katika klabu hiyo, na kuifanya kuwa timu inayoshinda taji kutokana na aina yake ya uchezaji inayoegemea kumiliki mpira na kusajili wachezaji wenye ubora zaidi.

Katika majira ya joto, nahodha wa Uswizi Granit Xhaka, mlinzi Alejandro Grimaldo na fowadi Victor Boniface walijiunga na kuthibitisha mafanikio ya timu.

Xhaka ametoa uongozi katika safu ya kiungo, Grimaldo aliongeza mabao na asisti kutoka kwa beki wa kushoto na mshambuliaji wa Nigeria Boniface amekuwa tishio kwenye safu ya ushambuliaji.

Leverkusen walinyakua taji, huku Boniface na Xhaka wakifunga mabao matatu kabla ya Florian Wirtz.

Mabadiliko ya Alonso yamemfanya avutiwe na vilabu vingine vikuu kote barani Ulaya haswa, Bayern Munich, Liverpool na Real Madrid lakini alitangaza mwezi uliopita kuwa atasalia Leverkusen msimu ujao.

"Hatukuzungumza sana kuhusu ubingwa kwenye chumba cha kubadilishia nguo lakini ilikuwa vichwani mwetu kwamba mwaka huu tunaweza kuwa mabingwa," Alonso alisema.

"Sasa lazima tufurahie wakati huu. Umekuwa msimu mkali kabisa hadi sasa na bado haujaisha. Hatuwezi kuisahau.Sasa hii iko nyuma yetu na bado tuna malengo makubwa msimu huu." Aliongeza

# Siri ya kupendwa wimbo wa 'Nawashukuru Wazazi' wa Sikinde

- **Mtunzi Gama asema aliutunga kukumbuka fadhila zao**
- **Awavulia kofia Omar 'Dulla', Pishuu kwenye ridhimu**



**Na Hamid Yassin**

UKIPATA fursa ya kuongea na mwanamuziki mkongwe na mahiri Abdallah Ally Gama, utafaidika kwa kuambiwa mengi muhimu.

Utafaidi kwa kuijua historia sahihi ya bendi kongwe ya muziki wa Dansi ya Orchestra Mlimani Park maarufu 'Sikinde Ngoma ya Ukae'.

Aidha, utapewa simulizi nzuri kwa kujua ni wapi bendi hiyo ilikoanzia. Vivyo hivyo utaelezwa kazi ambazo wanamuziki takriban 80 tofauti tofauti, walioipigia bendi hiyo tangu Novemba Mosi, 1978 jinsi walivyotokwa na jasho kiasi cha kuwafanya wawe mabingwa wa muziki Tanzania miaka kumi na mbili mfululizo.

Kumbukumbu hizo mbali ya kutakiwa kuwepo kwenye makabrasha ya ofisi za Mlimani Park, bali pia zimo kwenye kichwa cha Gama ambazo anaweza kukusimulia kwa ufasaha kama vile amezihifadhi kwenye kompyuta.

Jina la Abdallah Gama ambaye ndiye mtunzi wa wimbo wa 'Nawashukuru Wazazi', linaendelea kushika chati kwa kuwa mtunzi wa kibao bora mpaka sasa ndani ya Wanasikinde.

Ukweli huo unachagizwa na jinsi wimbo huo unavyoendelea kutesa hata baada ya kupita zaidi ya miaka 37 tangu ulipotungwa.

Mwandishi wa makala ya hivi karibuni alipata ukweli usio na kificho kuwa; Gama licha ya kukaa kando kwa kutoshiriki kuipigia bendi hiyo kwa muda mrefu, lakini 'ngoma' yake hiyo ndiyo bado inashikilia ubora wa kupendwa na wapenzi wengi ndani na nje ya nchi ikizizidi nyimbo zote ambazo bendi hiyo imewahi kutunga.

Gama almaarufu kama 'String Master' kutokana na udonyoaji wake maridhawa wa gitaa la rythim, anabainisha kuwa, alianza kuandaa mashairi ya wimbo wake huo alipokuwa nyumbani kwake enzi hizo Temeke Chang'ombe Mtaa wa Miteja, miaka ya 80.

Anasema baada ya kufika kambini alimuita pembeni mwimbaji nyota Hassan Rehani Bitchuka (bado yuko kundini Sikinde), kisha akamweleza azma ya kutaka kutunga maudhui ya wimbo huo.

Anaongeza kuwa, baada ya hatua hiyo magwiji watatu marehemu Michael Enock 'King au Teacher', marehemu Joseph Bartholemeo Mulenga 'Spoiler' na Bitchuka 'Stereo' waliukarabati wimbo huo kabla ya kujitosa kwenye Studio za iliyokuwa Redio Tanzania Dar es Salaam (RTD) sasa hivi linafahamika kama Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) kuurekodi huku ukienda sambamba na nyimbo nyingine tano ambazo zilikuwa zikijumuisha albamu yao ya pili.

Uelekeo kwa kiasi kikubwa limewiana kwa asilimia mia na kile ambacho Gama amekitamka kwa kauli yake wakati akizungumza na mwandishi wa makala haya kwamba, kwa nini aliamua kutunga wimbo huo ambao ulitokea kuchota hisia za wengi kisha kupendwa kila kona ndani na nje ya nchi hasa nchini Kenya.

Mkongwe huyo amefichua kuna siku ambayo haikumbuki kwamba, alijiwa na wazo moja alipojiuliza swali gumu iweje wazazi ambao ndiyo watu pekee wanaotuleta hapa duniani, wasahauliwe kwa wanamuziki wengi kutowatungia nyimbo za kuwaenzi japo kidogo kwa yale mema waliyotufanyia toka walipotuzaa, walipotulea, walipotusomesha na pengine hata pia walipotuwezesha kuoa ama kuolewa?

Gama aliona kuwa ni kama kuwakosea adabu wazazi kwa kutosifia fadhila zao, ama kwa vyovyote vile kuacha kuwatendea japo hata kutoa shukrani kwao huku yeye akijua fika kuwa, alikuwa ni mwanamuziki wa kiwango cha juu.

Kutokana na kupata mshawasha huo, Gama amesema alipata jibu moja tu. Kwamba, hakuwa na jinsi bali kutunga wimbo ambao aliamini kama ungetoka studio, basi ungetosha kuwa gumzo la nchi.

Kwa kauli yake, Gama amesema miongoni mwa wanamuziki walioshiriki kupiga na kutoa mchango mkubwa katika kibao chake hicho kilirekodiwa RTD ni mwanamuziki machachari Abdallah Omari 'Dulla' anayeishi Sweden hivi sasa.

Anasema Dulla alipata ajira ndani ya Sikinde kufuatia kupiga kwa ustadi gita zito la besi katika wimbo huo akiachiwa kwa hiari na mkongwe marehemu Abel Balthazar.

Gama amewataja wanamuziki Omar 'Dulla' na Mustapha Hamis 'Pishuu' wa Msondo Ngoma kuwa hao ndiyo pekee ambao wanamsuuza kutokana na ukung'utaji wao maridadi wa gita la ridhimu kushinda wote.

Mbali ya wimbo huo, vilevile Gama ndiye mtunzi wa nyimbo 'Khadija', 'Elimu ni ufunguo wa maisha', 'Wikiendi', 'Chenga ya mwili Dar es Salaam' na zingine kedekede.

> **Kutokana na kupata mshawasha huo, Gama amesema alipata jibu moja tu. Kwamba, hakuwa na jinsi bali kutunga wimbo ambao aliamini kama ungetoka studio, basi ungetosha kuwa gumzo la nchi.**

# Ras Nganyagwa katika mabonde na milima ya muziki-3



***Wiki iliyopita tuliona simuliza ya mwanamuziki mkongwe wa Reggae. Innocent Nganyagwa akisimulia jinsi alivyojitosa katika muziki na kupitia 'msoto' mkubwa na hatimaye kuanza kupata mafanikio ya kimuziki. Endelea kupata simulizi hii sehemu ya tatu ya kusisimua kupitia gazeti lako hili pendwa la Uelekeo.***

ILIHANIKIZA vilivyo kutokana na video alizonishuti Kaka Sadrus. Luguruni (Makondeko Six) nilipata marafiki wengi akiwemo Dweza Kolimba (Mtoto wa hayati Horace Kolimba) aliyeishi Kwembe na wanakijiji wengine wa Luguruni.

Niliowataja hapa leo ni miongoni mwa wachache kati ya wengi ambao kamwe siwezi kuwasahau, mathalan, Sadrus humwita kaka yangu na wakati ule ananishuti video hakuwa na familia bado lakini baadaye alipoasisi familia kila nilipokuwa nikimtembelea aliwaambia wanawe kwamba mimi ni baba yao mdogo, ingawa walistaajabu maana yeye Sadrus ni Mwasia mimi Rastaman.

Hatimaye Munisandesa (Muziki ni safari ndefu sana) ilianza kugatua vituo vya fanaka kwa sapoti za walioelewa ndoto nilizolenga hata kuwafanya wapinzani wengine kugeuka washitiri na kukubaliana na harakati, maana hata kama wangenizuia wasingeweza kwani ni sawa na kuzuia mawimbi kwa viganja kama nitakavyokueleza kwenye sehemu inayofuata ya IV.

**HATIMAYE NIKACHANGAMANA, NIKAINUKIA, NIKAKUBALIKA KIMUZIKI:**

Munisandesa-Muziki Ni Safari Ndefu Sana. Kutoka harakati zilizopita nilizokufahamisha katika sehemu zilizotangulia ya simulizi hii ya 'Muziki Ni Safari Ndefu Sana', kwenye mapito yangu kimuziki hatimaye milango ikafunguka kupitia wenye mapenzi mema maana dalili za kushikamana huonekana mapema.

Kaka yangu marehemu Mathias 'Mathew' Nganyagwa, ndiye alikuwa shabiki wangu na mfuasi wangu namba moja ndani ya familia aliyenikingia kifua kila walipotaka kupinga ndoto zangu. Mathias alifariki Mei 10, 1999 siku moja kabla ya siku ya kumbukizi ya kifo cha Bob Marley.

Kuinukia kwenye muziki kukaniweka mkabala na Wana-Reggae waliotangulia kimafanikio hapa nchini, nikafahamiana nao na Jeshi la Askari wa Reggae likaongezeka kwa idadi.

Nikafahamiana na Justin 'Cam' Samue Glaces Kalikawe wakati huo alikuwa akiishi mkabala na Shule ya Sekondari ya Tambaza jirani na Ofisi za STAMICO, mtu tuliyeondokea kufahamiana zaidi hata nilishawahi kufika nyumbani kwake Kitendaguro kule Bukoba Mjini mkoani Kagera wakati huo Mama yake Mzazi (Maribora Kashebo) alikuwa bao hai, pia nikafahamiana naye Bi Mkubwa huyo.

Mwingine niliyekuja kufahamiana naye ni kaka mkubwa Samuel Mreteni 'Jah' Kimbuteh niliyekuwa na kawaida ya kumtembelea nyumbani kwake Msasani Mtaa wa Ali Bin Said, alinisaidia sana mawaidha ya kudhibiti hamkani za maisha ya Uwenza (Nilikuwa napitia changamoto wakati huo) sanjari na kunielekeza namna ya kukabiliana na changamoto za maisha ya muziki.



Wapigaji wake nd'o walikuja kuwa wapigaji wetu baadaye wakiwemo akina Thom Nhigula na Hamisi Kambimtoni. Nikababahatika kukutana uso kwa macho na Lucky Dube alipokuja hapa nchini kwa ziara ya maonesho, sambamba na kina Empress Gypse Vancy (Mama Africa), Dj Ngomeley na Emsley Raimont Smith (Baba T) waliomiliki Kampuni iliyoandaa Matamasha ya Reggae hapa nchini ambako nilipata nafasi ya kutumbuiza.

Pia nikafahamiana na Kaka mkubwa Innocent Galinoma wakati huo tayari alishakuwa amehamia nchini Marekani alipo hadi sasa anapofanyia shughuli zake za muziki. Kaka Inno ambaye wengi walikuwa wakichanganya utambulisho wake nami tunatoka mkoa mmoja kwa asili (Iringa), hata vijiji vyetu vya asili Kalenga na Kaning'ombe vinakaribiana kwa umbali huku wote tukiwa kabila moja la Wahehe na sote tunafanya Reggae na wote ni Rasta.

Tangu tumefahamiana tumekuwa na ukaribu unaokiukia nasaba na ushirikiano kwenye 'maeneo mtambuka' ya kimuziki na kifamilia sanjari na nduguze wengine akiwemo Henry 'Jongo' Buti Jiwe a.k.a Mzee mwenzangu ambao ni watoto wa marehemu Mzee Steven Galinoma, ambaye aliwahi kuwa Mbunge wa Jimbo la Kalenga ambalo linajumuisha Kijiji changu cha pili cha asili Kiponzelo, kilichopo Kata ya Maboga wilaya ya Iringa Vijijini. Ushirikiano wangu naye nitaueleza zaidi kwenye sehemu zijazo za Simulizi hii.

Mambo kadhaa ya kimsingi yaliyoniinua ni pamoja na kutoa albamu yangu ya kwanza 'Money-Pesa' (1994) yenye 'Wimbo wa Taifa wa Reggae' (Gila) iliyorekodiwa Studio za Don Bosco, Upanga, hapa Jijini. Albamu ya Pili iliyofuatia 'Millioni 13' (1997) ilirekodiwa pia Don Bosco niliigubika mguso wa utetezi kwa watoto wanaokabiliwa na madhila mbalimbali.

Jina la Albamu limetokana na jina la wimbo 'Millioni 13' ambazo ni takwimu za Umoja wa Mataifa (UN) za idadi ya vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa mwaka kutokana na majanga mbalimbali yakiwemo yanayosababishwa na binadamu (Vita vya wenyewe kwa wenyewe).

Albamu iliyofuata 'Innocent' (2003) niliirekodi kwenye kiwango tofauti (Backyard Studio) kutokana na maendeleo ya kiteknolojia (Kidijitali) kupiga hodi nchini, ambayo ilinipa Mwendelezo wa kunyakua tuzo kwa kuwa albamu bora ya Reggae ya mwaka kwenye Tuzo za Taifa.

Albamu hii ilisababisha nijikite kufanya safari ya utafiti juu ya madhila ya watoto niliyoyaimba kwenye nyimbo zilizomo kwenye albamu hiyo. Jasiri haachi asili kwani kwa kila albamu nimehakikisha naweka wimbo mmoja wa Kihehe; Money-Pesa (Gila), Millioni 13 (Pandauli) na Innocent (Segito).

# Inter Milan watwaa ubingwa Italia

**Na Valensi Mbaga**



KIPINDI cha neema kwa Inter Milan kimeonekana wazi baada ya kutwaa ubongwa wa ligi kuu ya Italia Seria A msimu huu baada ya kuwachapa wapinzani wao wa jadi AC Milan bao 2-1.

Inter ilishinda ligi mara ya mwisho msimu wa 2020/21 lakini ilishindwa kuendeleza hilo katika miaka miwili iliyofuata, ikitazama Milan na Napoli wakishinda misimu ya 2021-22 na 2022-23 .

Wenyeji walianza mchezo kwa kumiliki mpira huku wakicheza kwa umakini mkubwa, lakini wapinzani wao wa Jiji la Milan, AC Milan walipata kipigo cha kwanza kufuatia shambuli lao la kwanza la maana.

Baadaye kona iliyopigwa na Dimarco ilikutana na Acerbi ambaye alikuwa na huru eneo la hatari na kupiga mpira wa kichwa uliompita kipa Mike Maignan.

“Tunajikuta katika hali ambayo haijawahi kutokea hapo awali,’” nahodha wa Inter Lautaro Martínez alisema. “Tulihitaji kutumia fursa hii, kwa sababu katika pande zote, uwanja wote ni wetu sasa.”

Baada ya kushinda mataji mengine nane akiwa mchezaji, Simone Inzaghi alitwaa taji lake la kwanza la ligi akiwa kocha.

“Kushinda ligi zikiwa zimesalia mechi tano au kushinda chini ya hapo zikiwa zimesalia mechi tisa, na kuifanya kuwa na uhakika kihisabati katika mchezo wa derby, hilo ni jambo litakalobaki kwetu kama historia,” Inzaghi alisema baada ya mchezo huo.

“Kila mtu alitoa mchango wake muhimu sana ili tuweze kufikia malengo kama haya.”

Wakati huu, imekuwa kampeni kubwa kwa vijana wa Inzaghi, huku washindi wa Scudetto wakiwa wamefunga mabao mengi zaidi kwenye Serie A huku pia wakijivunia safu ya ulinzi iliyo ngumu zaidi.

Kurudi kwa mchezji wao kinaraLautaro kuliimarisha mashambulizi ya Nerazzurri, na kufunga mabao 23 , huku Marcus Thuram na Hakan Calhanoglu wote wakifikia takwimu sawa.

Mfumo wa mabeki wa pembeni uliotumiwa na Inzaghi, ukiwa na uthabiti kutoka kwa Benjamin Pavard, Alessandro Bastoni na Stefan de Vrij kuwaruhusu Dimarco na Denzel Dumfries kusonga mbele, ulionyesha ufanisi zaidi katika kuwabatilisha wapinzani.

Kwa ushindi huu, Inter wanasonga mbele ya AC Milan katika mataji ya ligi ya Italia, wakiwa wametoka sare ya 19 kabla ya msimu huu huku Juventus wanaongoza kwa kutwaa ubingwa mara 36.

Zaidi ya hayo, Inter walikuwa wameshinda mechi tano zilizopita za derby, ikijumuisha mikondo yote miwili ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa mwaka jana na fedheha ya 5-1 dhidi ya Milan msimu huu kwenye Serie A.






# Minong’ono ya usajili Ulaya

## De Zerbi kumrithi Ten Hag Man United

**MANCHESTER, England**



MENEJA wa Brighton Roberto de Zerbi ndiye anayeongoza kuchukua nafasi ya Ten Hag ikiwa ataondoka Old Trafford, na Seagulls wanamfikiria kocha mkuu wa Burnley Vincent Kompany kama mbadala wake.

Hatima ya kocha Erik ten Hag itajulikana baada ya tathimini itakayofanywa na Mkurugenzi mpya wa Ufundi wa Manchester United, Jason Wilcox kabla ya klabu hiyo kufanya uamuzi kuhusu mustakabali wa Mholanzi huyo.

## West Ham wanamtaka Ruben Amorin

**LONDON, England**



WEST Ham wamepanga kufanya mazungumzo na kocha mkuu wa Sporting Lisbon Ruben Amorim, 39, huku hawajaamua iwapo wataongeza mkataba wa David Moyes msimu huu wa joto.

Haijabainika ni wapi Wagonga Nyundo hao wa London wataangukia kati ya Amorim na Moyes. Kocha wa zamani wa Wolves Julen Lopetegui pia anatajwa kuwa ni mshindani mkubwa kati ya wanaowania nafasi hiyo ya Moyes.

## Bayern Munich wamtupia jicho de Jong


**MUNICH, Ujerumani**



BAYERN Munich wanafuatilia hali ya mchezaji wa Barcelona Frenkie de Jong, ingawa mshahara wa kiungo huyo wa kati wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 26 unaweza kukatiza uhamisho wake.

## Al- Nasri yamwania De Bruyne


**RIYADH, Saudi Arabia**



KLABU ya Saudi Arabia Al-Nassr bado ina nia ya kumsajili Kevin de Bruyne wa Manchester City msimu wa joto na inatarajiwa kuwasiliana na kiungo huyo wa kati wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 32 hivi karibuni.

## Barcerona yaingilia dili la Arsenal kwa Alexander


**BARCORONA, Hispania**



BARCELONA wameingilia dili la Arsenal kutaka kumnunua mshambuliaji wa Newcastle United na Uswidi, Alexander Isak, 24, mwenye thamani ya pauni milioni 90, huku klabu hiyo ya Uhispania ikitarajia kufanya makubaliano huku Magpies wakitafuta kufuata sheria za usawa wa kifedha.

## Real Betis wamwinda Davis de Gea

**MADRID, Hispania**



REAL Betis wanalenga kumsajili mlinda lango wa zamani wa Manchester United na Uhispania David de Gea, 33, ambaye amekuwa mchezaji huru tangu kuondoka Old Trafford mwishoni mwa msimu uliopita.

Leo yetu ndiyo kesho yetu

Uelekeo Spoti

| Jumatano Aprili 24 - 30, 2024 |

# Simba yapiga chini ofa ya Lakred

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa Klabu ya Simba umetupilia mbali ofa ya timu ya MC Alger ya Algeria ya dola 375,000 sawa na zaidi ya shilingi milioni 960 kuhitaji saini ya mlinda mlango wao, Ayoub Lakred raia wa Morocco.

Habari kutoka ndani ya Simba SC zimeeleza kuwa, wameikataofa hiyo kwa sababu bado timu yao ina mpango wa muda mrefu na nyanda huyo mwenye umri wa miaka 28.

Timu ya kwanza kuhitaji huduma ya Lakred ilikuwa ni Wydad Casablanca ya nchini Morocco lakini sasa jirani zao MC Alger wamejitosa kumwania kipa huyo. Mbali ya Ayoub, pia beki kitasa wa timu ya Simba Enock Inonga Baka ameshaaga kwa mashabiki wa klabu hiyo ikidaiwa ameshasaini mkataba wa awali na timu ya AS FAR Rabat ya Morocco.



# Benchikha aundiwa zengwe Simba

## ● Wapambe wadai hajafanya lolote tangu atue Msimbazi

**Na Mwandishi Wetu**

IMEELEZWA kuwa, baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Ushauri ya Klabu ya Simba iliyoundwa na Rais wao wa Heshima, Mohamed 'Mo' Dewji hawamkubali kocha wao mkuu, Abdelhak Benchikha na wameanza kumuundia zengwe atimuliwe.

Kwa mujibu wa chanzo chetu kimefichua kwamba Kamati hiyo ya Ushauri yenye wajumbe 21, baadhi yao wameamua kutumia fursa waliyopewa ya kuishauri Bodi ya Wakurugenzi ya Simba na Sekretarieti ya klabu hiyo kumchimba Benchikha kwamba hana jipaya alilolingeza kwenye timu yao tangu aanze kuifundisha.

Wanadai bora kocha aliyetimuliwa baada ya kufungwa na Yanga 5-1, Mbrazili Roberto Oliviera Do Cormo 'Robertinho' kwamba, timu yao ilikuwa inafanya vizuri kuliko sasa ikiwa chini ya Benchikha.

Hata hivyo, wanachama wengine wa Simba wakiongozwa na magwiji wa klabu hiyo, Ismail Aden Rage na Jamhuri Kihwelo 'Julio' wamewapinga vikali wenzao hao kwa kudai Benchikha si tatizo Simba, ni kocha mzuri na mwenye wasifu mzuri katika soka la Afrika isipokuwa anaangushwa na aina ya wachezaji aliowakuta Msimbazi.

Rage ambaye ameshawahi kuichezea Simba miaka ya sabini na baadaye kuwa kiongozi wa klabu hiyo, amesisitiza kuwa, tatizo la Simba ni wachezaji wa hadhi ya kawaida walionao hususani wale wa safu ya ushambuliaji na wala siyo kocha.

"Mechi yetu na Yanga tulitakiwa kushinda, kabla watani wetu hawajapata bao, sisi washambuliaji wetu walishakosa goli mbili za wazi. Kipindi cha pili tukapoteza nafasi nyingine mbili, sasa hapa unamlaumu vipi kocha Benchikha?" Amehoji Rage.

Naye mchezaji wa zamani na kocha wa Simba 'Julio' amemtetea Benchikha na kwenda mbali zaidi kwa kutaka timu nzima ya Wekundu hao wa Msimbazi itimuliwe hasa wachezaji wao wa kigeni akidai hawana sifa za kuchezea kikosi chao.

"Tatizo la Simba si kocha ni wachezaji wanaosajiliwa holela kila msimu, timu inacheza vizuri kuanzia nyuma hadi mbele, inatengeneza nafasi za kufunga lakini wanashindwa kuzitumia! Sasa hapa unamtupiaje zigo la lawama Benchikha?" ameuliza Julio.



# Mechi ya Yanga, JKT yaota 'mbawa'

## ● Kisa, uwanja kujaa maji pomoni






**Na Mwandishi Wetu**

MECHI ya Ligi Kuu ya NBC baina ya wenyeji JKT Tanzania na mabingwa watetezi Yanga imeshindwa kufanyika jana kutokana na Uwanja wa Generali Isamuyo kujaa maji kufuatia mvua zinazoendelea kunyesha mfululizo kote nchini tangu juzi.

Kamisaa wa mchezo huo Kamwanga Tabwe alisema kuwa, baada ya ukaguzi uliofanywa na waamuzi wa mchezo huo walijiridhisha kwamba mechi hiyo isingewezekana kuchezeka kwani hata walipojaribu kudundisha mpira ulishindwa kudunda kama kanuni zinavyotaka.

Tambwe amesema wanalipeleka suala kwenye mamlaka za juu za uongozi ambao ndiyo wataamua mechi hiyo ichezwe lini na kwenye uwanja upi.

Timu zote mbili zilifika uwanjani na taratibu zote zilifuatwa ikiwemo kuzikagua na wachezaji kupasha moto misuli kabla ya waamuzi kutoa taarifa hiyo kwamba mechi isingewezekana kuchezwa kutokana na hali hiyo ya uwanja.

Wakati huo huo, Klabu ya Yanga imeeneza mabango maeneo mbalimbali ya Dar es Salaam yanayoonyesha ushindi wa mabao 7-2 dhidi ya watani zao Simba yaliyopatikana kwenye ushindi wa mechi mbili za msimu huu wa Ligi Kuu ya NBC.

Hii ni mara ya pili kwa Yanga kufanya hivyo, awali waliweka mabango hayo mwezi Novemba mwaka jana baada ya kuwafunga mahasimu wao bao 5-1 kwenye mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu.